

TAMTHILIA YA KILIO CHA HAKI NA ALAMIN MAZRUI

UTANGULIZI

Tamthilia ya '*Kilio cha haki*' iliandikwa na Alamin Mazrui mwaka wa 1981 kutoka nchini Kenya. Imechapishwa na 'Autolitho Limited' Nairobi Kenya. Inazungumzia juu ya mapambano kati ya waafrika na Wazungu. Wafanya-kazi wa kiafrika wanaongozwa na mwanamke jasiri-Lanina wanapigana na makaburu uso kwa uso ili waweze kujikomboa kutoka mikononi mwa wakoloni (*wazungu*). Vile vile, inafafanua dhahiri jinsi Mzungu anavyomtesa, anavyomdhalimu, anavyomnyonya, anavyomnyanyasa, anavyomtusu mwafrika hivi kumnyima haki zake.

Baadhi ya wahusika wanaopatikana katika tamthilia ya '*Kilio cha haki*' ni kama vile; Delamon (*Kaburu mwenye mashamba*), Shindo na Zari (*ambao wanamsaidia Delamon*), Lanina (*anayeongoza wahusika katika harakati za ukombozi*), Mwengo (*mume wa Lanina anayelilia mapenzi*), Baba (*babake Lanina*), Mama (*mamake Lanina*), Musa (*anayekubaliana na Lanina kujitoa mikononi mwa Delamoni*), Dewe (*anayefanyia Delamon kazi ngawa anafikiana na Lanina kujikomboa*), Makachero (*1 na 2*), Tereki, Pelekha na Matovu (*Viongozi wa chama kipya cha wafanyakazi wa Delamon*) na wengine.

UCHAMBUZI WA JALADA (KIFUNIKO CHA KITABU)

Jalada la tamthilia ya '*Kilio cha haki*' lina jina la mwandishi ambaye ni *Alamin Mazrui* kutoka nchini Kenya. Pia, jalada limepambwa na picha mbili za vichwa vya watu. Watu hawa wana uchungu mzima na hata wanatiririka machozi wakijaribu kuililia haki ambayo wamenyimwa na makaburu. Picha hizi zinaonyesha msimamo imara wa kuzipambania haki zao eti wajikomboe dhidi ya udhalimu, unyanyasaji, unyonyaji, ukandamizaji ambavyo vimewasakama.

Aidha, jalada limerembeshwa kwa kuzitumia rangi tatu, rangi nyeusi ambayo inadhihirisha Waafrika ambao wamo katika giza, vile kuwa hawajazinduka usingizini kujikomboa. Rangi nyekundu inadhihirisha hatari inayowakumba waafrika wakijaribu kujikomboa kama vile kutiwa kizuizini. Rangi ya kijani wastani imechukua sehemu kubwa kuionyesha amani inayojitokeza baada ya giza na hatari yaani uhuru wenye kila haki.

DHAMIRA YA MWANDISHI

Mwandishi wa tamthilia ya '*Kilio cha haki*' anadhamiria kuwaonyesha viongozi wa Afrika wanaojaribu kujikomboa dhidi ya udhalimu, unyonyaji, unyanyasaji, ukandamizaji ambavyo vyote vinafanywa na mzungu kumnyima mwaafrika haki zake. Mwanamke jasiri- Lanina anawaongoza wafanyakazi wenzake katika mashamba ya Bwana Delamon kuyaanza mapambano ili waweze kuepukana na mishahara duni, kutukanwa

katika kazi, udhalimu na mateso. Lanina anawazindua wafanyakazi wenzake katika usingizi wasioulalia au kuula na kuaanza mapambano.

UFUPISHO WA MAONYESHO KATIKA TAMTHILIA YA KILIO CHA HAKI

Utangulizi Chini ya mti (UK 1-6)

Katika onyesho hili, Dewe na Musa wameketi chini ya mti wakizungumzia juu ya mambo ambayo yamejitokeza katika gazeti. Dewe anaanza kusoma gazeti ambalo linaonyesha kwamba mwanamke Lanina ametiwa tena kizuizini akidaiwa kuchochea mgomo miongoni mwa wafanya-kazi wenzake. Musa anakasirika akisema kuwa Lanina wamemfitini na siku ya mgomo hakuwepo. Musa kwa hasira kuizidi ile ya kwanza anamfahamisha Dewe eti, kumpeleka Lanina mahakamani ni kuchemsha ari ya wafanya-kazi wengine kuendelea kugoma. Onyesho hili pia linaonyesha kuwa waafrika wanakatiliwa kwa kuwaletea mabunduki na majibwa kuwatafuna. Dewe anaonyesha kuwa Lanina analaumiwa bure eti ameuja ingawa hajaua mtu yeyote. Aidha, Dewe anafasiri kwamba sheria za kibeberu hazitekelezi haki bali kuwalinda wanyonyaji na rasilimali zao kwa mfano, msichana alitafunwa na majibwa ya mabwanashamba lakini bwanashamba hakutiwa kizuizini bali anaendelea kuishi raha mstarehe. Katika onyesho hili, tunaonyeshwa kwamba kamishana wa polisi Henderson anaapa eti hatapumzika hadi atakapowakamata wauaji. Katika mwisho wa onyesho hili, tunamwona mzee mkongwe analalamika juu ya mateso ya mzungu - wenzao na kuendeleza kazi ya Lanina.

Onyesho la 1 (uk7-14) – Katika ofisi ya Delamon.

Ofisini mwa Bwana Delamon, ana wasaidizi wake Zari na Shindo. Wote hawa wana hasira na wasi wasi, malalamiko yanaonekana katika meza na wafanya-kazi, wanaimba kwa sauti thabiti kwa sababu ya unyonyaji na udhalimu. Sauti za wafanya-kazi zinadhihirisha jinsi wanavyoteswa na kulemewa na mizigo mizito ya hasira na uchungu.

Katika onyesho hili, Delamon ana hasira kutokana na sauti za wafanya-kazi analaumu Zari na Shindo kwa kushindwa kumnyosha Lanina anayechochea mgomo. Delamon yuko kwenye bahari ya wasi wasi akisema kuwa maneno ya wafanyakazi si ya kutaka mshahara na kutaka nafuu kazini! Delamon anamwamuru Shindo kumpigia kamishana wa polisi Henderson ingawa Shindo simu inaanguka, Delamon anaishika na kumpigia mwenyewe akimwelezea eti wafanya-kazi wamegoma. Katika mazungumzo ya simu, sauti za wafanya-kazi zinasikika zikidai jasho, damu, haki na utu. Katika wasi wasi zaidi, anamwamuru Kimbo kuwaita Lanina na Tereki eti wajiadiliane. Baadaye, Tereki na Lanina anawakaribisha na kuwaita rafiki zake (*Delamon anatoa tabasamu la fisi mwenye njaa*) akisema kwamba amefurahi wamekuja. Anaambia Kimbo kuwaletea chai

lakini wanaikataa. Anawaambia kumfafanulia malalamiko, Tereki anajaribu kuyasema lakini anakatishwa na Lanina ambaye kwa imara anamwambia kwamba malalamiko yameshaletwa katika barua. Zari anawambia Lanina kuwa wao ndio viongozi wanaochochea migomo na kuwaita washenzi, ingawa anakemewa na Delamon.

Bwana Delamon anafasili kwamba amekuja na kujitolea kusaidia maendeleo ya Afrika lakini Lanina anamfichulia ukweli fika ati wamekuja masilahi na faida yao wenyewe. Sauti za wafanya-kazi zinasikika zikilalamika. Lanina na Tereki wanajaribu kwelekea mlangoni lakini wanakutana na askari mlangoni anawatia pingu.

Onyesho la 2 (uk 15-20) Katika ofisi ya polisi

Katika onyesho hili, Shindo na Kachero wameketi upande mmoja. Kachero ambaye ni kachero kweli anataka wafanyakazi wanaochochea mgomo wafukuzwe. Baadaye, askari wawili wanamleta Tereki na Kachero anamkaribisha na kumpa kiti. Shindo anajaribu kumshawishi kwa kumwambia eti Delamon ana huruma na angetaka aache migomo.

Shindo anaendelea na kumshawishi eti Bwana Delamon anamtaka awe kiongozi wa chama kipya cha wafanya-kazi ambacho ni cha kuchunguza malamiko ya wafanyakazi. Shindo anamwambia kuwa anaheshimiwa na Bwana Delamon na ndiyo sababu anataka kumnufaisha na kuwaacha wengine. Tereki anawafafanulia kwamba Lanina anapendwa sana na wafanya-kazi wengine na asiponufaishwa kama kurudishwa kazini, wafanya-kazi wengine waweza kulipuka.

Hatimaye, Shindo anamwomba kukubaliana na jambo la kunufaishwa peke yake ingawa yeye Tereki anawambia kumpatia muda wa kufikiria juu ya jambo hilo. Hapo wanampatia muda wa siku mbili, askari wawili wanakuja na kumchukua na kurudishwa chumbani mwake, Kachero anawashauri kutomwadhibu.

Onyesho la 3 (uk 21-28) – Katika ofisi ya polisi.

Onyesho hili linamwonesha Lanina katika polisi, ana makachero ambao wanamhoji na kumshawishi. Katika mashtaka haya, Kachero wa 1 anamwambia Lanina kwamba ameletwa kwa mara ya pili kwa kesi ile ile ya kuchochea mgomo. Mara ya kwanza katika shamba la Rhodeman na sasa Bwana Delamon.

Katika onyesho hili, tunaonyeshwa kwamba Lanina amekataa kushirikiana na Wazungu kwa mara ya kwanza na wana matumaini ya kushirikiana nao bila usumbufu wowote. Lanina anawaelezea fika kwamba yeye hapiganii dhidi ya udhalimu peke yake bali mgomo ni wa wafanya-kazi wote. Aidha, ni katika onyesho hili ambapo tunamwona Lanina anateswa na Kachero wa 1 kwa kumbinya kwa nguvu na vidole.

Waidha, Kachero wa 2 anamwuliza tena Lanina lengo lake lakini kabla ya kujibiwa Lanina anazabwa kofi linalomwangusha chini. Lanina mwanamke jasiri anaendelea na

kumwambia kwamba madhumuni ya wafanya-kazi ni kupigania haki zao za kikazi, na kupinga udhalimu wa Delamoni kama wanavyoimba katika nyimbo zao.

Baada ya kumshawishi na kuchoka, wanamwumiza kwa kumvuta masikio kwa nguvu. Tunamwona Lanina anasema kwamba Bwana Delamon na wenzake hawakuja kunufaisha waafrika bali kuinyonya nchi yao. Fauka ya hayo, anafafanua dhahiri kwamba kuna waafrika wanaofanya kazi katika mashamba makubwa lakini wanakufa kwa njaa, yaani hawali, hawanywi. Kachero wa 1 anamwambia Lanina kuwa angewaambia mapema, wangewapatia suluhisho akisema kwamba hilo ni jambo rahisi kuwapatia malipo mema. Mashaswishi haya yote anayafanya huku akimpapasapapasa minajili ya kumfanyia mapenzi lakini Lanina anaruka kwa hasira na kumwita mhuni jambo ambalo linamkera Kachero wa 1 na kutaka kumzaba kofi.

Migogoro inaendelea huku Kachero wa 1 akimsukumilia cheche za matusi Lanina akimwita Malaya. Baada ya mivutano hiyo, Kachero wa 2 anamwambia Lanina kushirikiana nao ili wampe nyongeza na kumpa cheo kidogo. Lanina naye anaerevuka na kuwauliza watakalowafanyia wenzake lakini kwa upumbavu wake Kachero wa 2 anamwambia kuwa hawawezi kumfanyia mpango kila mtu kwani dunia ni ya ubinafsi.

Kachero wa 2 anaendelea kumshawishi eti rafikiye Tereki ameungana nao na amepewa nyongeza na kurudishwa kazini, amepewa cheo na hivi wanamtaka Lanina naye ashirikiane nao. Lanina anakataa katakata kukubali oni la kwamba Tereki ameungana nao, anasema Tereki hawezi kuwasaliti na akiwa amefanya hivyo, lazima ameisaliti nchi yake.

Baadaye, Lanina anaachiliwa uhuru, anaondoka huku akiyahisi maumivu ya mapigo.

Onyesho la 4 (uk 29-35) – Nyumbani mwa Mwengo.

Mwengo mume wake Lanina ana wasi wasi nyumbani mwake, anavuta sigara. Nyumba yake ni ndogo yanye vitu vinavyohibitisha umaskini. Mara tu anamfungulia mlango Lanina anayetoka kifungoni anayekijaribu kupigania haki.

Mwengo anamkaribisha mkewe na matusi akimwambia kwamba ameisahau familia yake, amemsaheu mume, watoto wake kwa sababu wanakula chakula kibichi. Mwengo anamwambia Lanina ati ametiwa kizuizini mara ya pili kwa sababu zisizofahamika na kuiacha kando haja ya familia, anaendelea kumjulisha eti yeye hawezi kustahimili mambo hayo.

Lanina anamwambia mumewe kupoa moto huku akijaribu kumbebeleza mtoto wake Dida akimwonyesha mapenzi aliyoyakosa kwa siku kadhaa. Mwengo anasema peke yake Lanina anapolisha mtoto wake. Anasema kwamba mke huyo amekuwa kama amiri wa mabadiliko, anasema kwamba mkewe amezisahau mila na desturi za kikwao. Sasa ndiye anayejichungia familia.

Onyesho hili linaonyesha dhahiri mapigo ambayo yamemfikia Lanina jambo ambalo Mwengo anatambua baadaye, na kumhurumia. Anampapasapapasa usoni akimwambia '*pole*'.

Mwengo anaendelea kumwambia kwamba anajihatarisha na mambo yasiyomhusu ndwele wala sikio. Lanina naye anamwambia Mwengo kuwa yeye kujitoali watoto wake si jambo la ajabu, si makosa hayo.

Hatimaye, tunamwona Lanina anamfafanulia shida za wafanya-kazi akisema Mwengo naye ni miongoni mwa wanaokandamizwa na makaburu. Hivi anamshawishi kuwa washirikiane na wajitete dhidi ya udhalimu lakini Mwengo anakubali kama hakubali akimwambia, '*nitajaribu*'. Wanashikana mikono na kwenda kulala.

Onyesho la 5 (uk 36-42) Kijijini- nyumbani mwa Baba

Katika familia ya Baba na Mama, wazazi wake Lanina, Baba mwenyewe ana hasira kama mkizi, analaumu vijana wa siku hizi akisema wameacha mila zao na wanataka kuwa wazungu. Baba mtu ana hasira kwani mumewe Lanina (*Mwengo*) amemshtaki kwa kutoipatia muda familia yake, ameshughulikia mambo ya siasa sana na kutoijali familia yake. Anafikia kiwango cha kuwa na hasira nyingi sana, na anasema kuwa Lanina si mtoto wake. Mamake Lanina anajaribu kumtetea akisema Lanina ana kazi mjini na watu wanaowaletea habari mbaya wanamwonea kijicho wakimbandika dosari, anaendelea kusema, '*mkosa chema haachi kuguna*'. Baba anamwambia mama mtu kusema na mtoto wake.

Baada ya makabiliano hayo, Lanina anaingia akitoka kizuizini alikotiwa na makaburi, anakaribishwa na mamake anayemlilia kwa maisha machungu aliyoyapata huko, lakini babake yeye anakataa hata kumsalamia akisema, "*nikwambie usiniite baba, husikii? Ndiyo! Mimi sikuzaa Malaya!*" uk 37. Babake Lanina anjaribu kumwonya mamake eti amfunze adabu. Anasema, "*mimi ni dume kweli kweli*". uk3 8, anamwambia mamake kumfunza adabu, heshima na maana ya (*uuke*) ati akomeshe udume wake.

Baada ya hayo, mwanamke mamake Lanina anaanza kumfunza adabu na heshima. Anamwambia kwamba watu wameanza kusema kuwa amekuwa mchafu na hata mumewe anajipikia, anajinawishia watoto jambo ambalo linakera kulingana na utamaduni wao. Anamwambia ni sharti mke awe chini ya mume, amtii na amhudumie mumewe.

Mwishoni mwa onyesho hili, tunamwona Baba anajitokeza ameshika bakora mkononi. Ana cheche za matusi zilizochanganywa na hasira. Anawatesa wote kwa vipigo, anawafundisha adhabu ama adabu, Lanina anatoweka akiambiwa eti asirudi kwao na babake. Baba anamshika Mama akitaka kumrudisha kwa shangazi yake kuwa afundishwe tena kumtii mumewe.

Onyesho la 6 (uk43-48) Shambani mwa Delamon.

Katika shamba la Bwana Delamon. Wafanya-kazi waliomo Tereki, Matovu, Dewe, Musa na mfanya-kazi mwingine (MK) wana mivutano. Musa na Dewe wana maoni tofauti ya kumtetea Lanina anayepigania haki. MK anasema wao wamepewa nyongeza jambo ambalo linamnung'unisha Musa na kumwita mjinga. Dewe anajaribu kuwaingilia ili wasiendelee na ugomvi.

Tereki naye anamshabiki MK kuwa wamepewa nyongeza lakini Dewe anakataa usemi huo. Tereki, Matovu na MK wanadhani wamepewa nyongeza. Mivutano inaendelea ingawa Dewe ambaye ana nguvu anawaingilia katikati. Musa anawajulisha kuwa jambo la kuwapatia nyongeza linaweza kuwafanya kutolipwa 'overtime', na hata watalazimishwa kufanya kazi zaidi ya nyakati za kawaida.

Dewe kwa msimamo wake thabiti anasema jambo linalomsumbua ni Lanina kufukuzwa kazini japo amepigania masilahi yao wote, anapendekeza eti tafadhali wafanye jambo fulani. MK ana hofu na kusema yeye hawezi kwa sababu hataki kufukuzwa kazini yaani ana mke na watoto wanaomtegemea. Tereki, Matovu na MK wanaishia wakisema mambo ya Lanina hayawahusu.

Mwishoni mwa onyesho hili, tunamwona Dewe anaamua kuonana na Lanina kwa sababu wafanya-kazi wameshindwa kukubaliana yaani Dewe na Musa wanataka kumtetea Lanina lakini Tereki, Matovu, Pelekha na MK hawataki hilo.

Onyesho la 7 (uk 49-55) Nyumbani mwa Mwengo.

Katika onyesho hili, tunawaona Tereki, Matovu na Pelekha wanamtembelea Lanina kumliwaza juu ya kikomo alichokilalia. Lanina anawaambia kwamba katika hali ya mapambano hakuna hali ya kusikitika anasema *'tumenyimwa haki zetu, na ni sharti tupigane'*. Lanina anasema kwamba amepewa kazi na Mzee Ingeli ingawa ina mshahara mdogo lakini sio unaodunisha wafanya-kazi. Licha ya kuwa Tereki, Matovu na Pelekha hawamtaki Lanina achochee mgomo, wanajaribu kumshawishi eti aiache kazi ya mzee Ingeli na aungane nao. Wanamwambia kwamba Bwana Delamon ni mtu mwenye huruma na anataka washirikiane.

Lanina anakataa jambo la kusaidiwa na Delamon na baadaye, anagundua eti wamekuja kumshawishi. Lanina anamwambia fika Tereki eti ni msaliti. Hii ni kwa sababu, wametiwa kizuizini kwa kuchochea migomo lakini Tereki anamsaliti kwa kuyakubali maoni ya Delamon. Kwa hasira zaidi, anajaribu kuwafukuza ingawa Pelekha anamwambia kupoa moto, wanarudi kuketi. Tereki anamwambia kuwa shambani kumeanza kuwa na uhuru kidogo, kinachobaki ni kubadilisha siasa zao tu za kupigania haki zao. Anaendelea kumwambia kuwa nguvu na mizozo haifai.

Lanina anamjibu ya kwamba wafanya-kazi wa kiafrika hawawezi kujikomboa kwa sababu ya usaliti. Wote watatu yaani, Tereki, Matovu na Pelekha anawaita wasaliti. Katika mashawishi hayo, Mwengo mume wake Lanina anaingia na watoto wake anapowaona anapandwa na hasira, analeta bakora na kuwafukuza.

Baada yao kuondoka, ugomvi unaendelea kati ya Mwengo na Lanina. Lanina anapigwa na kupigika. Anaambiwa kutoleta wanaume katika nyumba yake. Watoto wake Lanina wanamkumbatia.

Onyesho la 8 (uk 56-65) Katika kioski ya Mzee Ingeli.

Onyesho hili linatendeka katika kioski ya Mzee Ingeli. Sehemu hii ni ya kuuzia uji (*biashara*). Lanina anaonekana katika kazi ndogo hiyo ambayo ameipata baada ya kufukuzwa na Bwana Delamon. Anasikilizwa na Mzee Ingeli akiimba wimbo wa ukombozi ambao unamvutia Mzee Ingeli na kuanza kumpigia makofi.

Mzee Ingeli anfurahia wimbo wa mjukuu wake na anamwambia kwamba wimbo wake ni wa ukweli kwa sababu naye anaona kunyanyaswa kunawafuata kama mkia wakati wote. Lanina anamwambia eti lazima kunyanyaswa, kudhulumiwa na kuumbuliwa huanzishwa na binadamu na kukomeshwa na binadamu na kwa hivyo, waanze mawazo ya kuinua tamaa na ari yao.

Watu watatu wanaingia wakiwa na lengo la kumwomba mapenzi. Lakini Lanina kwa imara anawambia kuwa anaye mume na hawezi kuingia katika hali ya mapenzi. Anaendelea kuwaelimisha kuwa waanze kuwaheshimu dada zao, wanastahili kuzinduka na kufahamu eti kunyanyasa na kudunisha wanawake kunarudisha nyuma ukombozi. Haya yote anayasema akiwa na hasira ambayo inatulizwa na Mzee Ingeli anayemwambia kuipatia uji mijitu hiyo. Baadaye, watu hao wanamsikitikia.

Dewe na Musa nao wamechukua muda mrefu bila kumwona, wanamkuta kwa Mzee Ingeli. Wanamwambia Lanina kuwasamehe kwa kutomtembelea lakini naye anasema wamefanya vizuri kwa sababu mume wake Mwengo ana wivu. Lanina anawaambia kwamba wasaliti (*Tereki, Matovu na Pelekha*) wamekuja kumshawishi eti abadilishe nia yake. Dewe, Musa na mtu 1, 2, 3 wanamshabiki kuendelea na mikakati ya kujikomboa ingawa mtu wa 4 yeye anaonyesha hofu.

Onyesho la 9 (uk66-72) Katika ofisi ya Delamon)

Katika ofisi ya Delamon, Delamon na Shindo upande mmoja na Tereki upande mwingine. Wafanya-kazi waliogoma wanaimba nyimbo za kujikomboa. Nyimbo hizo ni za siasa.

Delamon amechanganyikiwa, anasema wafanya-kazi hawawezi kuupata mshahara kama wake yaani "*watu wote hawawezi kuwa sawa duniani*". Tereki anamwambia kwamba baadhi ya wafanya-kazi wanaoendelea kuimba wameonana na Lanina.

Delamon anamwambia Shindo kumpigia simu Kamishna Henderson. Hii ni kwa sababu anataka Lanina achukuliwe hatua asimvunjie biashara. Shindo anampigia simu ikiwa mikono yake inatetematemema halafu Delamon anampokonyana kumpigia. Anamfananua kuwa migomo imekuwa mikubwa zaidi. Bado sauti za wafanya-kazi zinasikika zikilalamika.

Tereki woga unamzidi kiasi, anataka kutoroka lakini anazuiliwa na Delamon akisema “*sasa mambo yamechacha, wewe ndiyo unataka kutoroka!*” Anamwambia eti atabaki mpaka wamalize haja yao.

Dewe na Musa wanaingia, Tereki msaliti anapowaona anatazama chini. Delamon anawauliza malalamiko yao, anaendelea kusema kwamba hawana shukrani, amewapeni ruhusa ya kuunda chama, nyongeza, Lanina ameikataa kazi mwenyewe lakini bado hawajatosheka. Musa anamwambia ukweli kwamba hawataki wasaliti kuongoza chama chao yaani anamjulisha kuwa chama chao ni sharti kifuata sheria za masilahi ya wafanya-kazi. Delamon anamwambia, wawakilishi hao (*wasaliti*) ndio ambao wamewasaidia kupewa nyongeza.

Ghalibu ya hao, sauti za wafanya-kazi zinasikika, ving'ora vya polisi vinasikika. Musa anamwambia Dewe kuwa wenzao wanapigwa na polisi vibaya. Anamwambia eti waendeni kuwasaidia. Delamon anawafahamisha kuwa Lanina ameshikwa na nguvu zao zimekwisha.

Mwishoni mwa onyesho hili, tunamwona Musa, Dewe na wafanya-kazi wengine wanaanzisha ugomvi, Dewe anapokonya mtu mmoja gongo, anamwendea Delamon. Kwa hofu zaidi, Delamon, Tereki na Shindo wanarudi kinyumenyume, Dewe, Musa na watu watatu wanawafuata, Dewe yuko karibu na Delamon, anainua gongo hilo akiuliza; Dewe: *Damu imwagikeee!*

Watu: *Imwagikeee!*

Onyesho la 10 (uk 73-77) Gerezani.

Lanina amejikunja pembeni gerezani, mara mlango anapoufungua, anaingia askari. Askari mwenye hisia za kinyama, anaahidi kumsaidia kwa kumnunulia sigara na chakula mara tu akikubali kumpa mapenzi. Tunamwona anamwendelea kumbusu na kumpasulia nguo kwa ushurutisho. Lanina mwanamke jasiri anajitetea kwa kumpiga teke (*goti*) kwenye sehemu za siri, askari anayahisi maumivu machungu. Kwa sadfa, watu walichokuwa anafanya, askari anapepesapepesa macho kwa haya.

Wakili na Kachero wa 2 wanamwambia Lanina kuwa anashtakiwa kwa mauaji ya Bwana Delamon, Bwana Shindo na rafiki yake Tereki. Lanina anashangaa kuyasikia hayo. Lanina anawajulisha kuwa siku hiyo hakukuwepo. Wanaendelea kumwambia kwamba, ndiye aliyechochea migomo ambayo imewafanya Dewe, Musa na wafanya-

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211
kazi wenzake kumaliza maisha ya watu. Wakili anamwambia eti atapelekwa mahakamani.

Lanina anawaelezea kwamba ametiwa ndani ya gereza na kwa hiyo hajui yoyote ya kuua. Kachero wa 1 anamkumbusha kuwa maneno yake ya uchochezi katika kioski ya Mzee Ingeli, na kumpiga mtu yule aliyeshindwa kukubaliana naye ndivyo vinavyosababisha vifo vya watu watatu hao.

Wakili anamwambia Lanina kwamba ingekuwa bora kuepukana na mambo ya siasa, akae nyumbani awalee watoto wake na mumewe. Wanamwambia kuwa siasa ni mchezo mchafu- mchezo wa wanaume tu. Lanina anawambia kwamba, siasa kweli ni mchezo mchafu lakini unatakiwa kusafishwa.

Mwishowe, Lanina anajuta kuzifanya kazi zisizo na thamani, akimwahidi mamake mpendwa eti atarudi nyumbani.....

PLOTI YA TAMTHILIA YA KILIO CHA HAKI

Ni msuko, mtiririko au mfuatano wa matukio au matendo katika kazi ya kifasihi. Tamthilia ya *'Kilio cha haki'* ina ploti sahili kwa sababu tukio moja linasababisha jingine kutoka mwanzoni hadi mwishoni. Ploti ya *'Kilio cha haki'* inaonyeshwa kama ifuatavyo; Tamthilia ya 'Kilio cha haki' inaanza tukiwaona Dewe na Musa wanasoma gazeti na kuonyesha kuwa mhusika Lanina ametiwa kizuizini kwa kuchochea mgomo miongoni mwa wafanyakazi. Wanaonyesha kukasirika juu ya unyanyasaji wa makaburi na wanakubariana kurudi nyumbani na kuwaamsha wafanya-kazi wengine kuendeleza kazi ya Lanina. Vile vile, tunaendelea kusikia sauti za wafanya-kazi wanaolalamikia haki zao wakiimba nyimbo kupigania haki. Lanina na Tereki wanaletwa ofisini mwa Delamon na kushawishwi eti watapewa nyongeza lakini yeye Lanina kwa imara anakataa. Baadaye, tunawaona, Kachero na Shindo wanamshawishi Tereki peke yake, kujiunga nao, na anawaambia kumpa muda wa kufikiria hayo. Vile vile, baada ya Lanina kukataa mashawishi, tunamuona katika polisi ananyanyaswa na Kachero wa 1 na wa 2 kwa kupigwa makofi, mateke na kumwendea kumnyang'anya kimapezi. Kuongeza hapo, tunamuona Lanina anaachiliwa kwenda nyumbani ambapo anakaribishwa na matusi ya Mwengo mumewe kwa kumlaumu kutojali familia yake. Baada ya hayo, tunamuona Lanina pia ametembelea wazazi wake kijijini ambapo tunamuona babake mkali kama moto anamkataa na kusema eti si mwanake, anamwita Malaya, binti ya shetani kwa sababu ameuacha utamaduni na kujipeleka katika shughuli za kujipigania uhuru. Kisha, tunawaona Dewe, Musa, MK, Tereki na Matovu mjadalani wa kumwokoa Lanina lakini wengine wanakataa ila Dewe na Musa. Halafu, Tereki, Pelekha na Matovu wanamwendea nyumbani kumshawishi lakini anakataa kusimamisha ugomvi. Lanina anapata kazi katika kioski ya Mzee Ingeli ambapo Dewe

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211
na Musa wanamkuta kumpa pole. Baada ya muda, tunamuona Tereki ameungana na Delamon. Shindo na Delamon wana wasi wasi wanajaribu kumpigia kamishna wa polisi ili aje atulize wafanya-kazi. Wakiwa hapo, Dewe na Musa wanaingia wakiwa na hasira wanawauwa. Hatimaye, tunamwona Lanina gerezani akipambana na askari anapojaribu kumbaka. Tamthilia inaishia tukimwona katika huzuni akiahidi kurudi nyumbani kumwona mamake mpenzi ama akiwa hai au la.

MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA YA KILIO CHA HAKI

- Maudhui ni kile kinachosemwa katika kazi ya fasihi.
- Vile vile, maudhui ni jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa pamoja na mtazamo wa mwandishi juu ya mawazo hayo.
- Maudhui hujumuisha mawazo pamoja na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma msanii hadi akatunga na kusanii kazi ya fasihi.
- Kwa upande mwingine, maudhui ni ile mada inayoendelezwa na wahusika katika mazungumzo yao.
- Kwa ufupi, maudhui ni ule ujumbe muhimu msomaji anaoupata katika kazi ya mwandishi.

Kwa kurejelea tamthilia ya '*kilio cha haki*', maudhui yafuatayo yanapatikana;

1. Kilio.

Kilio ni ari ya mhusika kupata kitu fulani akitumia mwelekeo maalumu kupata kitu hicho. Kilio ndiyo mada kuu ya tamthilia hii ambayo inajitokeza miongoni mwa wahusika. Kwa mfano, wahusika wengi wanalilia haki zao, mathalani;

- ❖ Kwanza, kuna kilio cha haki ya kujikomboa dhidi ya unyanyasaji, udhalimu na mateso. Kwa mfano, tunawaona Lanina, Dewe, Musa na wafanya-kazi wengine wanapigania haki zao. Mathalani, tunamwona Lanina anaambia wateja katika kioski ya Mzee Ingeli kuwa kudunisha wanawake kunarudisha nyuma ukombozi (*uk 58*).
- ❖ Aidha, kuna kilio cha kuhifadhi utamaduni. Kwa mfano, tunamwona Mwengo mumewe Lanina analilia haki ya kupikiwa chakula yaani, anasema eti si utamaduni wao mume kujipikia chakula na kuwalea watoto. Na hiki kinaonyesha kilio cha haki ya utamaduni (*uk 32*).
- ❖ Vile vile, wafanya-kazi wanalilia mishahara minono. Kwa mfano, tunamwona Lanina anasema kwamba makaburu wanawadhulumu, wanatumia nguvu zao, wananyang'anya ardhi yao na kuinyonya nchi yao kwa gharama ndogo isiyokuwa na thamani. Hivi basi, kilio cha mishahara minono (*uk 13*).
- ❖ Kilio kadhalika ni cha usawa wa kijinsia. Kwa mfano, tunamwona Lanina anapigania usawa wa kijinsia wakati anapokataa mambo ya kiutamaduni.

Mathalani, tunamwona anamwuliza Mwengo, “*utamaduni ni kitu gani?*” (*uk 32*).

Vile vile, anaendelea kusema eti hatauacha utamaduni utilie sing’enge ukweli wa maisha yake na ukweli wa ubinadamu wake, na kwa hiyo, hiki ni kilio cha usawa wa kijinsia (*uk 33*).

- ❖ Jambo kadhalika, tunawaona Dewe na Musa wana kilio cha kumpigania Lanina kuachiliwa. Kwa mfano, tunawaona wakikubaliana kurudi kwao kijijini na kuwaamsha wafanya-kazi wenzao kichinichini na kuendeleza kazi ya Lanina (*uk 6*).
- ❖ Waaidha, Delamon naye analilia amani miongoni mwa wafanya-kazi. Kwa mfano, baada ya wafanya-kazi kugoma, tunamwona ana wasi wasi na baadhi yao anawashawishi kuwapa nyongeza na vyeo eti wasiendelea na malalamiko. Mambo haya lazima yanathibitisha kuwa anataka amani (*uk 43*).
- ❖ Fauka ya kilio, wafanyakazi wana kilio cha haki ya kupata chakula. Kwa mfano, tunamwona Mzee Mkongwe analia kuwa njaa imewazunguka (*uk 5*). Juu ya haya, tunamwona Musa analia kwa njaa inayowasumbua yaani wanashindana na mbwa na mapaka waking’ang’ania makombo yanayotupwa na watu, na hivi ni kweli kuna kilio cha kupigania haki ya kupewa chakula (*uk 1*).
- ❖ Ghalibu, Mwengo analilia haki ya kupendwa na mkewe Lanina. Kwa mfano, Mwengo analilia mapenzi akidai kuwa Lanina amemaliza muda mrefu bila kuonekana nyumbani, na kwa hiyo haijali familia yake (*uk 29*).
- ❖ Isitoshe, kuna kilio cha kuzuia unyang’anyaji wa mapenzi. Kwa mfano, wanawake wanachukuliwa kama chombo cha kumstarehesha mume. Kwa mfano, tunawaona askari na Kachero wa 1 wanataka kumbaka Lanina lakini anajaribu kujitetea. Kwa mfano, anampiga askari goti katika sehemu zake za siri (*uk 73*).
- ❖ Pia, watoto nao wanalilia mapenzi ya mama yao. Kwa mfano, Dida na Badi wanatunzwa na baba yao pekee kwa sababu mama yao amechukuwa muda mrefu bila kuwaona (*uk 30*).

2. Migogoro.

Migogoro ni ugomvi, chuki unaojitokeza miongoni mwa wafanya-kazi (*wahusika*) kwa mfano;

- ❖ Migogoro wa kupuuza utamaduni kwa mfano, tunamwona Mwengo anagombana na Lanina eti amepuuza utamaduni wa kumpikia. Vili vile, Mama naye anagombana na Baba juu ya kupuuza utamaduni kwa mfano, tunamwona Baba anamwambia mkewe kutunza mwanawe (*uk 37*).

- ❖ Vile vile, kuna mgogoro kati ya Kachero wa 1 na Lanina. Kwa mfano, Kachero wa 1 anavutana na Lanina yaani anatia vidole vyake kwenye mabega ya Lanina na kumbinya kwa nguvu, Lanina analia kwa maumivu akijaribu kujikupua, lazima huu ni mgogoro (*uk 22*).
- ❖ Hali kadhalika, mgogoro kati ya Lanina, Wakili, Kachero wa 1 na Kachero wa 2 unaosababishwa na kutiwa kizuizini kwa Lanina. Kwa mfano, wanamshtaki kwa kuua Delamon, Shindo na Tereki akiwa katika kioski ya Mzee Ingeli akisema maneno ya kutisha (*uk 75*).
- ❖ Mgogoro mwingine unajitokeza kati ya Askari na Lanina. Kuna mvutano kati ya Askari na Lanina unaoletwa na tamaa ya Askari akitaka kumshurutisha katika mapenzi ingawa tunamwona Lanina akimpiga goti katika sehemu zake za chini. Tendo hili nalo linadhihirisha mgogoro(*uk 73*).
- ❖ Mgogoro kati ya Musa, Dewe na Delamon ambao unasababisha kifo cha Delamon, Shindo na Tereki. Kwa mfano, tunamwona mtu, Dewe na Musa wanakamata magongo na mwishowe wanamwaga damu. Kuuliwa kwa watu watatu kunaonyesha mgogoro (*uk 72*).
- ❖ Vile vile, tunaona mgogoro kati ya Musa, Dewe na mfanya-kazi(MK). Kwa mfano, tunaona MK anafurahia nyongeza na vyeo vinavyopewa na baadhi ya wafanya-kazi jambo ambalo linamkera Musa anamrukia na kumvamia ingawa Dewe anajaribu kuwatenganisha (*uk 44*).
- ❖ Mgogoro mwingine unaonekana kati ya Lanina na Delamon kwa sababu ya unyanyasaji na udhalimu.Mathalani, tunamwona Lanina anakabiliiana na Delamon na kumwambia uso kwa uso eti makaburu wamekuja kunyang'anya ardhi yao, kuinyonya nchi yao kwa gharama isiyo na thamani, hivi kuonyesha mgogoro (*uk 13*)
- ❖ Waaidha, mgogoro kati ya Lanina na wazazi wake unaonekana katika tamthilia hii kwa mfano, tunamwona babake Lanina anamkaribisha na cheche za matusi kwa sababu ya kuuchukua muda mrefu katika kupigania uhuru na kupuuza familia yake. Kwa mfano, hapikii chakula mumewe, mwishowe tunaona Baba anawadhibu wote wawili kwa kipigo kikali ingawa Lanina anatoweka (*uk 42*)
- ❖ Bila shaka, nyimbo za wafanya kazi na malalamiko vinaonyesha mgogoro. Kwa mfano, wafanya-kazi wanamgomea Delamon na kuanza kupiga kelele wakitaka nyongeza jambo ambalo linamtelea Lanina kufungwa jelani (*uk 1*).
- ❖ Fauka, kuna mgogoro wa kimapenzi katika ya Mwengo na mkewe Lanina. Kwa mfano, tunamwona Mwengo akimnung'unikia Lanina kwa kuchelewa kufika

nyumbani mapema. Kwa mfano, tunamwona, Mwengo anasema ndiye anayejiipikia watoto, anajifulia nguo (uk 32)

- ❖ Bila kudanganya, tunaona mgogoro baina ya Mwengo na Lanina, Pelekha, Tereki na Matovu ambao wamekuja kumshawishi eti afikiane na Delamon. Kwa mfano, tunaona Mwengo anashika bakora na kuwafukuza halafu anampiga Lanina (UK 54)

3. Usaliti.

- ❖ Hii ni hali ya kumtendea mtu kinyume kulingana na makubaliano. Kwa kurejelea tamthilia ya *Kilio cha haki*, maudhui ya usaliti huonekana pale ambapo Tereki ambaye anafungwa na Lanina kwa kuchochea mgomo. Kwa mfano, tunamwona Lanina akisema, *'kumbe mmekuja hapa kunishawishi niungane nanyi katika kuwasalati wafanya-kazi wenzetu! Tereki! Hata wewe Tereki!'* Bila shaka, hiki kinaonyesha usaliti (UK51)
- ❖ Pia, shindo na Tereki nao ni wasaliti ambao wanakubali uongozi wa chama kipya cha wafanya-kazi na kuwanyanyasa wenzao, mathalani, tunamwona Musa anamwambia Delamon eti hawataki tena hao wasaliti kuwa viongozi wa chama chao. Hivi lazima huonyesha maudhui ya usaliti (69)
- ❖ Aidha, usaliti unaonekana wakati ambapo Tereki, Matovu na Mfanya-kazi (MK) wanamtetea Demalon wakimsihi eti amewapa nyongeza, na kuwafanya viongozi, kwa mfano tunamwona Dewe anasema eti hizo ni siasa za kisaliti. Bila ya shaka' hiki kinaonyesha maudhui ya usaliti katika tamthilia ya *'kilo cha haki'*(uk47)

4. Dhuluma na Mateso.

Dhuluma ni hali ya kumnyima mtu haki na kumfanyia vibaya. Maudhui haya yanajitokeza katika njia zifuatazo;

- ❖ Kwanza kabisa, Sauti za wafanya-kazi zinaimba kujiokoa juu ya udhalimu. Kwa mfano, wanaimba wakisema kwamba wamateteseka kama fahali, wanalemewa mzigo wa maisha na kudidimizwa kwa uzito, matunda ya jasho yana sumu chungu unaoleta mauti. Maneno haya na mengine yanaonyesha udhalimu(uk 7).
- ❖ Fauka, Lanina naye anaonyesha kuwa waafrika wamedhulumiwa na Delamon. Mathalani, anasema Delamon ametumia nguvu zao, amenyang'anya ardhi yao, ameinyonya nchi yao kwa gharama ndogo isiyokuwa na thamani Lazima huu ni udhalimu(UK 13-14).
- ❖ Vile vile, Uk 40 unaonyesha udhalimu kwa mfano, Laniina anatuonyesha kuwa babake ni mkulima ambaye anadhulumiwa yaani analima na mavuno

yanamwedeza vizuri lakini makaburu wanampatia bei rahisi, hususa katika mahindi yake, jambo ambalo linaonyesha udhalimu.

- ❖ Aidha, tunamwona Musa akisema kwamba, bei za vyakula katika *Canteen* wamezongeza. Pia, anaonyesha eti wanafanya kazi kama mashine zaidi ya nyakati za kawaida lakini hawapewi 'overtime'. Haya yote bila udanganyifu yanaonyesha dhuluma(UK 45).
- ❖ Kwa upande wa mateso, yanaonyeshwa katika UK 42 ambapo Babake Lanina anamfukuza nyumbani mwake akimlaumu kuisaliti nchi yake. Vile vile, anachukua bakora na kumpatia kipigo, ingawa Lanina anatoweka na kipigo kinapewa mamake. Mama anapigwa na kuangushwa chini huku akilia na kupiga mayowe. Na kwa hiyo, mateso ni maudhui katika tamthilia ya '*kilio cha haki*'.
- ❖ Kando na hayo, Mwengo pia anamtesa Lanina anapomkuta akizungumza na Matovu, Pelekha na Tereki. Kwa mfano, tunawaona wanatoka mbio na baadaye, Lanina anapigwa na kuanguka huku watoto wao wakilia. Kipigo kama hiki kwa ukweli kinaonyesha maudhui ya mateso(UK54).
- ❖ Waaidha, ukurasa wa 22 unamwonyesha Kachero wa 1 akimtesa Lanina yaani anamshawishi kuungana nao lakini anapokataa, Kachero wa 1 anamtia vidole vyake kwenye mabega na kumbinywa kwa nguvu akiyahisi maumivu. Juu ya hayo, UK 23 unaonyesha Kasherero wa 1 akimvuta Lanina masikio kwa nguvu jambo linadhihirisha mateso.

5. Umaskini

Umaskini ni hali ya kukosa mali na fedha za kutosha. Umaskini unaonekana katika tamthilia ya '*kilio cha haki*' kupitia njia zifuatazo;

- ❖ Umaskini unadhihirishwa na maneno ya Musa. Kwa mfano, tunamwona akisema eti waafrika wengi wameanza kuishi kinyama, mathalani wanashindana na mbwa na mapaka waking'angania makombo yaliyotupwa na watu. Hali kama hii inaonyesha umaskini wenyewe(UK1).
- ❖ Ghalibu, mavazi ya Mzee Mkongwe yanaonyesha umaskini kabisa. Kwa mfano, amevalia matambara. Vile vile, tunamwona analalamikia njaa ambayo inamsakama. Hivi kweli vinaonyesha umaskini wa hali ya juu(UK 5).
- ❖ Umaskini kadhalika unajitokeza katika UK wa 29 ambapo nyumba ya Mwengo ni kama chumba au kibanda, yenye kochi moja bovubovu, yenye meza ndogo ina viti viwili, kando ya chumba kuna sufuria chache, masigiri na visahani. Hali ya namna hivi inahakikisha umaskini(UK 29).
- ❖ Isitoshe, umaskini unaonekana mionгани mwa waafrika ambao wananyanyaswa na makabuburi, kama vile; kuwalipa mshahara duni. Kwa mfano, tunamwona

Lanina akilalamikia umaskini unaowalalalia yaani anajiuliza *'itakuwa vipi? itakuwaje? Nikiwa na njaa na matambara mwilini, nimefanya kazi zisizo thamani.....'* Maneno haya na mengine yanathibitisha umaskini kwa dhati.

6. Uzalendo.

Ni hali ya mtu kuipenda na kuwa tayari kuifia nchi yake. Licha ya kwamba, tamthilia hii ni ya *'kilio cha haki'* kuna wahusika wanaopigania haki zao hivi wanaonyesha uzalendo, kama vile;

- ❖ --Mhusika Lanina ni mzalendo ambaye kwa uthabiti anapigania uhuru eti aweze kujikomboa. Kwa mfano, tunawaona Tereki, Pelekha na Matovu wanamshawishi eti aungane nao lakini anagundua kuwa ni usaliti, na mwishowe anawambia ukweli ati wafanya-kazi wa kiafrika hawajaweza kujikomboa kwa sababu ya wasaliti kama wao, halafu anasema yeye yuko tayari kuuondoa udhalimu wa ubepari(UK 53).
- ❖ Mahojiano kati ya Mzee Ingeli na Lanina yanaonyesha uzalendo mathalani, Lanina anamwambia Mzee Ingeli ukweli kuwa unyanyasaji, udhalimu vyote huanzishwa na binadamu na hukomeshwa na binadamu. Pia, anapendekeza kuwa, mwenge wa kutaka mabadiliko lazima uendelee kuwa ndani yao, na vivi hivi ni maudhui ya uzalendo(UK56-57).
- ❖ Vivi hivi Lanina ni mzalendo ukiangalia UK wa 33. Kwa mfano, tunamwona anamwambia mumewe (*Mwengo*) ati hamu yake imeishaamka kutafuta ukweli ilikofichika na hatapumzika mpaka afike. Maneno kama haya yanaonesha msimamo wa uzalendo.
- ❖ Msimamo kadhalika wa uzalendo unaonekana katika uk wa 31 ambapo Lanina anamwambia Mwengo, *'..... Wewe ni mfanya-kazi kama mimi. Unajua taabu zetu na tunavyodhulumiwa. Na kukomesha mambo haya ni lazima tupigania haki zetu; ni lazima tuwe na msimamo thabiti'*. Ukweli ni kwamba, haya yanadhihirisha maudhui ya uzalendo.
- ❖ Dewe, Musa na wafanyakazi wengine nao lazima wanaonekana kama wazalendo, kwa mfano, Dewe na Musa wanaonekana wakitetea Lanina anapotiwa kizuizini kwa sababu amechochea mgomo wa kupigania uhuru. Hali kama hii inaonekana katika UK wa 13 ambapo sauti za wafanya-kazi zikisikika kuwahimiza wapigania haki, kwa mfano, wanasema, *'njooni basi, njooni tusafishe njia*'. Kwa ukweli kuna uzalendo kama maudhui katika tamthilia ya *'Kilio cha haki'*.

7. Utamaduni / Mila na desturi.

Mila na desturi ni kufanya mambo kufuatana na mazingira, kaida na tabia za jamii. Mambo haya huwa na kanuni fulani na huweza kuzusha balaa yakifanywa kinyume. Kwa kurejelea tamthilia ya *'Kilio cha haki'* maudhui hujitokeza;

- ❖ --Katika Uk wa 32, unaonyesha kuwa Lanina amezitupa mila za kwao yaani hawezi kumpikia Mwengo na watoto wake, amejigeuza kuwa dume. Kwa mfano, tunamwona Mwengo akilalamika ya kwamba Lanina anakuja nyumbani akiwa amechelewa. Vile vile, Mwengo ndiye anayepika chakula, tunamwona anamwambia Lanina eti ameacha utamaduni kwa sababu kulingana na utamaduni wao, mwanamke ndiye anayestahili kumpikia mumewe. Na kwa hiyo, hiki kinaonyesha maudhui ya utamaduni.
- ❖ Juu ya utamaduni, Baba, babake Lanina anaeleza kuwa Lanina amegeuka kuwa mzungu, anataka kuwa mume kabisa. Anaendelea kutwambia kwamba kila kiovu hulaaniwa kulingana na jinsi walivyotunzwa na babu zao. Hivi vyote vinaonyesha utamaduni.
- ❖ Aidha, tunamwona Mamake Lanina anamfunza mambo ya -utamaduni, mathalani, anamwuliza, *'Si umefunzwa kuwa mke daima awe chini ya mume? Lazima amtii na amhudumie mumewe!'* Anaendelea kumwambia eti wamemfunza hayo tangu utoto wake. Pia, anamwambia eti fikra za kujilinganisha na mumewe ni za kihalifu ambazo zinaharibu mila zao, na kwa hiyo, haya yanafafanua maudhui ya utamaduni(UK 41).

8. Vifo.

Ni hali ya kupoteza maisha. Katika tamthilia ya *'Kilio cha haki'* vifo hupatikana;

- ❖ Katika uk wa 75 ambapo wakili anamwelezea Lanina kuwa Bwana Delamon, Shindo na rafikiye Tereki wameuawa katika harakati za kupigania haki miongoni mwa wafanya-kazi. Wahusika hawa wanauliwa na Dewe na wenzake.
- ❖ Bila shaka, Lanina anafafanua eti waafrika hawali, hawanywi kwa sababu ya udhalimu unaojitokeza na baadaye wanafia katika mashamba makubwa ya Bwana Delamon kwa sababu ya njaa, vivi hivi ni maudhui ya vifo(UK 25).

9. Ukoloni.

- ❖ --Ni hali ya watu kutoka nchi mbalimbali kuja na kuitawala nchi nyingine kiuchumi na kisiasa. Kwa mfano, Bwana Delamon anahakikisha maudhui ya ukoloni yaani anasema kuwa amejitolea kuja kusaidia maendeleo na kuwanufaisha waafrika kwa kuwapa kazi ingawa tunawaona Dewe, Musa, Lanina na wanya-kazi wengine wanalemewa na ukoloni halafu wanaupinga(UK 13).

10. Uasherati / Umalaya / Ukahaba.

- ❖ Uasherati ni hali ya kufanya mapenzi hobelahobela au kuwa na mpenzi mwingine nje ya ndoa. Kulingana na tamthilia hii, uasherati unaonekana wakati Askari anapomvamia Lanina kumfanyia mapenzi kwa ushurutisho. Mathalani, anajaribu kumbusu na kumpasulia nguo ingawa Lanina anjitetea kwa kumpiga goti kwemye sehemu zake za chini. Ni kweli huu ni uasherati (UK 73).
- ❖ Ghalibu ya hayo, Kachero wa 1 anathibitisha umalaya katika tamthilia ya '*kilio cha haki*'. Kwa mfano, tunamwona Kachero wa 1 anampelekea mikono mabegani na kuanza kumapasa Lanina, Lanina anaruka kwa hasira akimwambia eti asimwite Malaya. Haya yote lazima yanaonyesha uasherati (uk 23).
- ❖ Waaidha, umalaya unaonekana katika kioski ya mzee Ingeli yaani tunamwona mtu wa tatu katika UK wa 57 anamwomba Lanina mapenzi, kwa mfano, anasema, '*..... mtu kama mimi naweza kukupenda sana*', kauli hii lazima inaonyesha umalaya.

11. Ukatili.

Ni hali ya kukosa huruma. Kwa mujibu wa tamthilia ya '*kilio cha haki*', ukatili umechukua ngazi ya juu, kwa mfano;

- ❖ Tunamwona Musa akilalamikia ukatili wa makaburu (*wazungu*), kwa mfano, anasema eti wazungu wanaleta mabunduki na majibwa ya kuwatafuna, mathalani, anaonyesha kuwa kuna msichana wa kishamba ambaye ametafunwa-tafunwa na majibwa ya bwanashamba kwa sababu ya kupitia katika shamba la mzungu igawa kesi hiyo inaachwa shingo upande. Na kwa hiyo, ni kweli kuna maudhui ya ukatili katika tamthilia ya '*kilio cha haki*' (UK 3).
- ❖ Hali kadhalika, Mwengo naye anaonyesha ukatili, kwa mfano, tunamwona anamrukia Tereki, wanaanguka chini na kuanza kuminyana. Vile vile, tunamwona Mwengo akimwadhibisha Lanina kwa kumzaba gongo kwa sababu amekuwa anazungumza na wafanya-kazi wenzake. Hivi vyote vinaonyesha ukatili (UK 54).
- ❖ Babake Lanina naye ni katili kwa mfano, tunamwona anamtusu mtotowe Lanina akimwita malaya. Juu ya hayo, anaonekana akisukuma mke wake kwa teke na anamwangusha chini kuonyesha ukatili kamili.
- ❖ Ukatili mwingine unaonekana katika ukurasa wa 22 ambapo kachero wa 1 anamtesa Lanina anapopomtilia vidole vyake kwenye mabega yake na kumbinya kwa maumivu, Na kwa hiyo, ni kweli kuna maudhui ya ukatili katika tamthilia ya '*kilio cha haki*'.

12. Uvutaji sigara

Hii ni hali ya mtu kuvuta sigara na kutumia dawa za kuibua hisia za ukali. Wahusika wengi wanavuta sigara katika tamthilia ya *"kilio cha haki"* kwa mfano;

- ❖ Musa anapozungumza na Dewe anavuta sigara. Kwa mfano, anavuta sigara huku akitazama angani(UK 1).
- ❖ Fauka, Delamon naye ni mvutaji sigara .Kwa mfano, anapotiwa na wasiwasi kwa sababu ya kusumbuliwa na wafanya-kazi, anatoa kiko chake anajaribu kukiwasha lakini kinamshinda(UK 10).
- ❖ Mhusika kachero wa 1 naye anavuta sigara. Mathalani, UK wa 21, unaonyesha dhahiri kachero wa 1 akitoa paketi ya sigara mfukoni na kuishika baina ya vidole. Anaendelea kuiwasha anavuta na kuwachilia moshi Lanina kwa nguvu na kwa hiyo, ni uvitaji sigara.
- ❖ Pia, Mwengo naye anavuta sigara kwa mfano, UK wa 29, unamwonyesha chumbani mwake amekaa juu ya kochi, anavuta sigara kwa sababu ya wasiwasi.
- ❖ Katika hali sambamba, Lanina mwenyewe anaonyesha kuvuta sigara. Kwa mfano, anaonekana akichukua sigara zilizopo mezani, anatoa moja na kuiwasha lakini kwa hasira mwengo anaivuta sigara hiyo kutoka mdomoni mwake. Na kwa hiyo, kuna maudhui ya uvutaji sigara(UK 29 na 31).
- ❖ Isitoshe, UK wa 33 unamfafanua Lanina kama mvutaji sigara yaani tunamwona anatoa sigara nyingine na kuiwasha. Anaendelea kuivuta kwa nguvu, na kutoa moshi mwingi huku akiutazama unavyopaa hewani, na hiki lazima huonyesha maudhui ya uvutaji sigara.
- ❖ Babake Lanina naye ni mvutaji sigara, kwa mfano, tunamwona katika kibanda chake akinusa (ugoro) chupani-kwa kweli ni wazi kusema ati *'kilio cha haki'* kama tamthilia ina maudhui ya uvutaji sigara(UK 36).
- ❖ Uvutaji sigara kadhalika unaonekana katika UK 43 ambapo tunamwona Tereki naye anavuta sigara. Kwa mfano, Tereki anatoa pakiti ya sigara, anawakaribisha wenzake, anawapa Matovu mfanya-kazi (MK), wanachukua na kuziwasha. Bila shaka, ufafanuzi huu unaonyesha uvutaji sigara.

13. Nafasi ya mwanamke/ hadhi ya mwanamke/usawiri

Nafasi ya mwanamke ni jinsi mwanamke anavyoonyeshwa na kusawiriwa katika jamii. Na kwa hiyo, kulingana na tamthilia ya *kilio cha haki*, mwanamke anasawiriwa kwa njia zifuatazo;

- ❖ Kwanza, mwanamke anasawiriwa kama mzazi. Kwa mfano, UK wa 30 unamwonyesha mwanamke Lanina ana watoto na mume. Kwa mfano, Lanina ndiye anayemzaa Dida ambaye anaonekana katika onyesho la 4 ukurasa wa

30. Vile vile UK wa 54 unamwonyesha Lanina akiwa na watoto wawili mathalani, tunamwona watoto wake wanamkimbilia na kumkumbatia, na hivi kuwa mzazi.

- ❖ Juu ya hayo, mamake Lanina ambaye anaitwa Mama naye anachukuliwa kama mzazi ambaye anamzaa na kumlea. Kwa mfano, tunamwona anampatia mawaidha katika (Uk 40-41).
- ❖ Hali kadhalika, mwanamke lazima anasawiriwa kama mpenda umoja. Kwa mfano, Lanina anamwambia Delamon kwamba mjadala wowote juu ya malalamiko yao ni lazima ufanywe na watu wanaowawakilisha na hiki wazi kinaonyesha umoja(UK 12).
- ❖ Juu ya umoja vile vile, UK wa 26 unaonyesha wazi kwamba mwanamke Lanina ni mpenda umoja, kwa mfano, tunamwona akimwambia kachero 2 wa pumbavu akisema, *'usinihonge kwa kunijaza na fikira za ubinafsi ama tupate sote au tukose sote!'*
- ❖ Kuongezea umoja, UK wa 35, unamwonyesha akimshawishi mumewe Mwengo kuwa waelewane na wasaidiane kwa ajili ya kupambania uhuru na bila shaka maneno haya yanamsawiri mwanamke kama mpenda umoja.
- ❖ Pia, mwanamke anasawiriwa kama mzalendo kwa sababu, yuko tayari kuifia na kuipigania haki chi yake yaani Lanina anasema, *'Delamon ndiye bwana na sisi ni watumwa katika nchi yetu wenyewe!.....La ikiwa ni lazima tunyonywe basi ni afadhali tunyonywe kwa malipo mema zaidi'*
- ❖ Uzalendo pia huonekana katika UK wa 57 yaani Lanina anamfafanulia Mzee Ingeli kuwa kunyanyaswa, kudhulumwa, na kuumbuliwa huanzwa na binadamu na kukomeshwa na binadamu na kwa hiyo, anaedelea kumwambia eti mawazo ya majaaliwa yanastahili kuuliwa ili wafaulu na hivi ni kumsawiri mwanamke kama mzalendo.
- ❖ Aidha, mwanamke anasawiriwa kama mwenye mapenzi ya dhati kwa mfano, anaonyeshwa mwanamke Lanina kama mwenye mapenzi yaani anamkumbatia mtotowe Dida halafu anamshika mkoni kwenda kumlaza kitandani.
- ❖ Kuna mapenzi kati ya Lanina na Ingeli ambayo ni thabiti mathalani, Lanina anapofukuzwa na Delamon kazini, Ingeli anampatia kazi. Juu ya hayo, tunamwona Mzee Ingeli akiwaambia wateja wa uji *'nisimwone mtu yeyote akimgusa mjukuu wangu, au atakiona cha mtema kuni'* lazima haya ni mapenzi kati yao wawili
- ❖ Vile vile, Lanina anawapenda watoto wake na Mwengo yaani tunamwona akiambia wakili kuwa awaelezee na kuwajaza habari kuwa anaweza kufia

gerezani. Bila shaka, hiki kinaonyesha kuwajali watu wa familia yake hivi mapenzi ya mwanamke.

- ❖ Mwanamke mamake Lanina naye ni mwenye mapezi yaani tunamwona akimtetea mwanawe Lanina dhidi ya matusi ya babake. Mathalani, tunamwona anamwambia eti amewatia wasiwasi na tangu aondoke, chakula kimewashinda kula. Hivi kuonyesha mapenzi(*UK 36*).
- ❖ Kando na mapenzi, mwanamke anasawiriwa kama mpigania haki za wafanyakazi wenzake , Kwa mfano, UK wa 12 unamwonyesha Lanina kwa uthabiti akilalamikia wafanya – kazi wenzake. Pia, tunamwona akimfafanulia mumewe eti kukomesha mambo ya udhalimu miongo mwao ni kupigania haki zao na kuwa na msimamo thabiti. Vile vile, Lanina anapigania haki, kwa mfano, anasema kwamba hamu yake imeshaamka katufuta ukweli ilikofichika, na kwa hiyo ni mpigania uhuru(*UK 31-33*).
- ❖ Waaidha, mwanamke anasawiriwa kama mchochezi wa migomo. Kwa mfano, UK wa 2, unaonyesha kuwa Lanina wa Muyaka, mwanamke aliyekuwa mfanyakazi katika shamba maarufu la Bwana Delamon, ametiwa tena kizuizini kwa kuchochea mgomo uliosababisha mauaji ya manokoa watatu wa shamba hilo. Lanina ana chochea mgomo ili waepukane na udhalimu wa makaburu hivi basi ni mchochezi wa migomo.
- ❖ Isitoshe, mwanamke anasawiriwa kama mfanya-kazi hodari. Kwa mfano, UK wa 2 unaonyesha Lanina akifanya kazi katika shamba la Bwana Delamon kabla ya kufukuzwa. Katika hoja sambamba, baada ya kufukuzwa na Delamon, tunamwona anapewa kazi nyingine ya kuuza uji katika kioski ya Mzee ingeli hivi kweli ni mfanya- kazi hodari.
- ❖ Hali kadhalika, mwanamke anasawiriwa kama mlezi. Kwa mfano, mamake Lanina anamlea kwa kumpa mawaidha juu ya utamaduni. Mama anamshauri kuwa mke daima, awe chini ya mumewe, kumtii na kumhudumia mumewe. Ukweli ni kwamba, malenzi haya yanamsawiri mwanamke kama mlezi(*UK 41*).
- ❖ Kuongeza hapo, Lanina anawalea watoto wake, kwa mfano, tunamwona anamlea mtotowe Dida kwa kumpeleka kitandani, na kwa hiyo, mwanamke anashauriwa kama mlezi(*UK 30*).
- ❖ Ghalibu ya hayo, mwanamke anasawiriwa kama shujaa/jasiri Lanina ni shujaa yaani yuko tayari kuifia nchi yake kwa hali yoyote. Kwa mfano, ushujaa wake unaonekana katika UK wa 73 ambapo anajitetea dhidi ya Askari anayejaribu kumbaka, anampiga goti katika sehemu zake za siri. UK wa 49 pia unaonyesha

ushujaa wa Lanina kwa sababu tunamwona akiwaambia Tereki, Matovu na Pelekha eti yeye hataki pole zao wakati wanapokuja kumliwaza.

- ❖ Juu ya ushujaa wa Lanina, ni mwanamke ni jasiri, kwa mfano, tunamwona anakabiliana uso kwa uso na Delamon, akimwambia eti wamekuja kudhulumu waafrika kwa kutumia nguvu zao, kunyanga'nya ardhi yao na kuinyonya nchi yao. Na kwa hiyo, mwanamke anasawiriwa kama shujaa(UK 13).
- ❖ Fauka, mwanamke anasawiriwa kama mvumilivu.Lanina anavumilia hali mbaya na matendo maovu katika tamthilia ya *'kilio cha haki'*. Kwa mfano, anavumilia mateso ya Kachwero wa 1 anayemvuta masikio kwa mguvu(UK 23).
- ❖ Vile vile, tunamwona Kacero wa 1 anamtia vidole vyake kwenye mabega yake Lanina na kumbinya kwa nguvu sana. Aidha, katika gereza, Lanina anateseka vibaya na Askari ambaye anataka kumnyanga'anya kimapenzi. Haya yote yananyesha uvumilivu UK 22.
- ❖ Kuongeza hapo, Mamake Lanina naye ni mvumilivu, kwa mfano, tunamwona, anavumilia mapigo ya mwewe na matusi yasiyo na kikomo UK 36-42. Ni ukweli, kuna kumsawiri mwanamke kama mvumilivu.
- ❖ Bila shaka, mwanamke anasawiriwa kama mweye kutilia maanani katika utamaduni. Kwa mfano, tunamwona Mama, mamake Lanina anamwelimisha mtotowe mambo ya utamaduni. Mathalani, anamwambia eti kuitamaduni ni sharti mke ampikie mumewe chakula, awe chini ya mumewe, amtii na amhudumie mumewe. Hivi vyote, vinamwonyesha mwanamke kama mtu wa kutllia maanani katika utamaduni (UK 41).
- ❖ Jambo kadhalika, mwanamke ni mwenye msimamo dhabiti/ lengo thabiti. Katika tamthilia hii, mwanamke hawezi kubadilikabadilika kimawazo , kwa mfano, katika Uk wa 13, Tereki anapjaribu kuzungushazungusha maneno akimwelezea Delamon, Lanina anamwambia eti asiutilie nguvu uongo, yeye anamwambia ukweli ati makaburu wamekuja kunufaisha masilahi yao badala ya masilahi ya waafrika, na kwa hiyo ana msimamo thabiti.
- ❖ Juu ya msimamo thabiti, tunamwona Lanina katika UK wa 57 ambapo mtu wa 3 anapomjaribu kimapenzi anamkataa katakata akimwambia eti ana mume. Anaonyesha kuwa hayapendi mapenzi yasiyo na mipango, hivi kuonyesha lengo thabiti.
- ❖ Bila kudanganya, mwanamke ni mvutaji sigara. Katika UK wa 33, tunamwona Lanina akiwa nyumbani na Mwengo anatoa sigara nyingine na kuiwasha, anaivuta kwa ngavu, na kuutoa moshi mwingi huku akiutazama unavyopaa angani, na ni kweli ni mvutaji sigara.

- ❖ Aidha, UK 49 unamwonyesha mwanamke Lanina kama mvutaji sigara akiwa na Tereki, Matovu na pelekha. Kwa mfano, tunamwona baada ya kuwakaribisha, anatoa sigara, anaiweka mdomoni na kuiwasha halafu anaivuta, hivi lazima ni kumsawiri kama mvutaji sigara.
- ❖ Waaidha, mwanamke ni mpenda usasa kwa mfano, tunamwona Lanina anataka kujisahaulisha na utamaduni wa kwao, yaani anataka kujisahaulisha/kujilinganisha na mumewe Mwengo. Mathalani, anamwachia kazi ya kupika, kulea watoto. Kwa mfano, katika UK wa 41, tunamwona akisema eti akichelewa kutoka kazini, Mwengo hupika yeye, vile vile, anasema eti hakuna ubaya wowote, Mwengo kuitumikia aila yake na hivi kweli ni kupenda usasa.

14. Biashara

- ❖ Biashara nikazi ya kuuza na kukunua bidhaa kwa ajili ya kupata mapato. Katika tamthilia ya *'kilio cha haki'* kuna baadhi ya wahusika ambao wanafanya biashara. Kwa mfano, Mzee Ingeli anafanya biashara ya kuuza uji na chai ili apate pesa. Mathalani, tunamwona anamwambia Lanina *'ipatie makopo ya uji na itatosheka'*(UK 57)
- ❖ Aidha, Bwana Delamon naye anafanya biashara chafu ya kununua nguvu za waafrika kumfanyia kazi katika mashamba yake kwa mshahara duni. Kwa mfano, tunamwona ananyanyasa wafanya-kazi kwa kuwapatia mshahara mdogo. Uhakika unaonekana katika UK wa 66 ambapo anasema eti Lanina ni punda kwa sababu amekataa kazi yenye malipo duni, na anataka kumvunja biashara yake. Na hivi ni kweli kuna maudhui ya biashara.

15. Mapenzi ya dhati

- ❖ Ni hali ya kuwa na upendo na kutakiana mema miongoni mwa wahusika. Kuna mapenzi kati ya Mwengo na Lanina ukiacha hitilafu zao kando. Kwa mfano, tunamwona Mwengo ahamhurumia Lanina wakati wa mateso yake na kusema *'kumbe.....wamekutesa huko!* Baadaye tunamwona anamsikitikia sana akimpa pole' na ukweli haya ni mapenzi katika UK wa 31.
- ❖ Bado juu ya mapenzi, Lanina ana mapenzi ya watoto wake. Kwa mfano, UK wa 30 unamwonyesha akimkumbatia mtotowe Dida na kumshika mkono kwenda kumlaza kitandani, na bila kudanganya hiki kinaonyesha mapenzi.
- ❖ Vile vile, mapenzi yanaonekana kati ya Lanina na mamake. Kwa mfano, tunamwona Mama anamtetea dhidi ya matusi na mateso ya babake. Haya yanaonekana katika UK wa 36. Juu ya hayo, tunamwona Mama anamwambia kwamba amewatia wasiwasi, na tangu aodoke chakula kimewashinda kula. Ni ukweli haya ni mapenzi katika tamthilia ya *'kilio cha haki'*.

- ❖ Fauka ya mapenzi, Mzee Ingeli naye lazima anampenda mjukuu wake Lanina. UK wa 57, unathibitisha mapenzi kati ya Mzee Ingeli na Lanina mathalani, baada ya Lanina kufukuzwa kazini mwa Delamoni, Mzee Ingeli anampatia kazi katika kioski yake na vile tunamwona anaambia wateja ati ‘ *nisimwone mtu yeyote akimgusa mjukuu wangu au atakiona chamtema kuni?*’ kauli hii bila kudanganya inaonyesha mapenzi.

16. Ukulima

- ❖ Ni hali ya kulima na kufuga mifugo. Katika tamthilia ya ‘*kilio cha haki*’ ukulima unaonekana katika UK wa 2 ambapo tunamwona Bwana Delamon ana shamba maarufu na wafanya-kazi wengi sana. Makaburu wana mashamba mengi ambayo wanayatumia kudunisha waafrika kwa kuwatumia kwa nguvu zisizo na malipo mazuri.
- ❖ UK wa 40 pia unathibitisha maudhui ya ukulima kwa sababu tunamwona Lanina anamfafanulia mamake kuwa, baba yake ana kishamba, anapanda mahindi. Mavuno yakimwendea vizuri, makaburu wanayanunua kwa bei naafu na ukweli ni maudhui ya ukulina.

17. Unyonyaji

- ❖ Ni tabia au hali ya mtu, kikundi cha watu kupokea malipo makubwa kutoka kwa nguvu za wafanya-kazi. Makaburu wanaoongozwa na Delamon wananyonya waafrika ambao wanawapatia bei duni kwa mavuno yao. Kwa mfano, tunamwona Lanina anaelezea kuwa babake, analima mahindi na anapata mavuno mazuri lakini anapewa malipo ya kiasi cha chini, na hivi ni unyonyaji.
- ❖ Waaidha, maudhui ya unyonyaji huonekana katika UK wa 25, ambapo Lanina anafafanua kuwa wazungu wanainyonya Afrika kwa kuwapa wafanya-kazi mishahara midogo ukilinganisha na nguvu zao. Mathalani, tunamwona Lanina analalamika akisema kuwa ikiwa ni lazima wanyonywe basi ni afadhali wanyonywe kwa malipo mema zaidi, na kwa hiyo ni maudhui ya unyonyaji.

18 Malalamiko

- ❖ Ni hali ya watu au mtu kujillia kwa ajili ya kuokoa maisha yake au yao. Kwa mfano, katika tamthilia ya ‘*kilio cha haki*’ wahusika wengi wanalalamika, mathalani, UK wa 8 unaonyesha sauti za wafanya-kazi wakilalamikia hali mbaya ya makaburu, tunasikia sauti zao zikisema kuwa wamezinduka.
- ❖ Vile vile, wafanya-kazi katika shamba la Delamon wanalalamika kwa kunyanyaswa, kunyonywa na kudhulumiwa na Delamon, kwa mfano, katika UK wa 9, tunawasikia wakisema,

‘Nivudishie jasho langu!

Nirudishie damu yangu !

Nirudishie haki yangu!

Nirudishie utu wangu'.Bila shaka, shairi hili linaonyesha maudhui ya malalamiko.

19. Ubinafsi

- ❖ Ni hali ya kujipendeleza mambo bila kujali maisha ya wengine. Katika tamthilia ya *'kilio cha haki'* kuna wahusika ambao wamejazwa na ubinafsi, kwa mfano, tunamwona Kachero wa 2, wakati anapomshawishi Lanina kushikiriana nao, anasema eti *'hatuwezi kumfanyia mpango kila mtu. Hii ni dunja ya ubinafsi'* ingawa Lanina anakataa akisema kwamba Kachero wa 2 asimhonge na kumjaza fikira za ubinafsi. Ni ukweli kuna maudhui ya ubinafsi.
- ❖ Pia, maneno ya Matovu yanathibitisha maudhui ya ubinafsi. Kwa mfano, tunamwona akisema, *'Lazima tupigania nafsi zetu kwanza, tujipatie vyeo, halafu tutaweza kuwasadia wenzetu'* Maneno haya lazima yanaonyesha ubinafsi(UK 53).

20 Ubepari

- ❖ Ni hali ya mtu au nchi kuwa na pesa, mali, biashara ambavyo huongozwa na mtu binafsi. Kwa mfano, katika tamthilia ya *'kilio cha haki'* Delamon ni bepari kwa sababu ana mashamba na biashara ambavyo anatumia kuzalisha pesa nyingi, mathalani, anawatumia waafrika kama wafanya-kazi kumsadia kupata pesa kupitia kuwafanyisha kazi na kuwalipa mishahara midogo (UK 7).

21. Uongozi / Siasa.

Ni hali ya kuwa na mamlaka ya kuongoza ukitumia sheria. Kwa mfano, katika tamthilia hii kuna uongozi mwingi sana, kama vile.

- ❖ Bwana Henderson ni kiongozi ambaye ni kMishna Mkuu wa polisi, kwa mfano, UK wa 2 unamwonyesha katika gazeti akimshtaki Lanina kwa kuchochea mgomo miongoni mwa wafanya-kazi na hiki humsawiri kama kiongozi hivi kuthibitisha maudhui ya uongozi.
- ❖ Bila shaka, Bwana Delamon naye ni kiongozi .Kwa mfano, tunamwona katika ofisi yake kama mkurugenzi mwenye wasiwasi zinazothibitishwa na maneno ya Shindo. Kwa mfano, Shindo anasema ati hawawezi kuzifahamu siasa za kibeberu yaani Delamon amekataa kuajiri wafanya-kazi wengine akisema kufanya hivyo ni kuharibu mambo(UK 7).
- ❖ Waaidha, kuna maudhui ya uongozi katika UK wa 43 kwa mfano, wafanya-kazi wamepewa ruhusa ya kunda chama. Mathalani, Tereki, Matovu na Pelekha wamechaguliwa kuwa vongozi wa chama hicho na kwa kweli ni maudhui ya uongozi.

22. Ushujaa/ujasiri.

- ❖ Ushujaa ni hali ya mtu kutenda bila woga na kuwa tayari kuikabili hali mbaya ya *'kilio cha haki'* yaani UK wa 73, unamwonyesha Askari akimshawishi Lanina kukubaliana nao lakini Lanina anakataa. Kwa mfano, tunamwona anampiga goti kwenye sehemu zake za siri anapotaka kumfanyia mabaya kwa sababu amekataa kukubaliana nao.
- ❖ Juu ya hayo, Dewe na Musa nao wanaonyesha maudhui ya ushujaa, kwa mfano, wanakabiliana na Delamon ofini mwake ya kibeberu. Mathalani, UK wa (71-72) unamwonyesha Dewe akisema *'.....tulinyosha mikono yetu kijinga, mkatutia pingu. Na sasa tutatumia nguvu zetu wenyewe kuzivunja....'* Mwishowe, tunamwona Dewe anashika gongo na kumzaba Delamon. Matendo haya yote bila shaka, yanadhirisha ushujaa.
- ❖ Kuongeza hapo, Lanina anaonyesha ujasiri wake katika UK 22. Kwa mfano, Kachero wa 1 na 2 wanamshawishi kuacha kuchochea migomo na kukubaliana na Delamon, lakini yeye habadili nia yake ya kupigania uhuru. Kwa mfano, tunamwona anakabili hali ngumu ya mateso kama vile, kuvutwa masikio, kubinywa kwa nguvu, kupigwa makofi na kadhalika lakini anahakikisha kuwa kuna maudhui ya ushujaa katika tamthilia ya *'kilio cha haki'*

23. Ubaguzi

- ❖ Ni hali ya kupendelea upande mmoja na kutopendelea upande mwingine. Kwa mfano, katika tamthilia ya *'Kilio cha haki'*, Delamon amasababisha ubaguzi kwa mfano, tunamwona akisema, *' watu wote hawawezi kuwa sawa duniani'*. Hivi amewapatia madaraka Makachero, Wakili, Tereki, Matovu na kuwabagua Lanina Musa, Dewe na wafanya-kazi wengine. Na kwa hiyo, kutengwa kwa wafanya-kazi hao kunaonyesha maudhui ya ubaguzi (UK 66)

24. Usasa.

- ❖ Ni hali ya kupendelea mambo ya sasana kuyapuuza yale ya ukale. Kwa mfano, tunamwona Mwengo akilalamikia Lanina kwamba ameitupa kando familia yake mathalani, Mwengo ndiye anayepika chakula, analea watoto. Mwengo anamwambia Lanina kuwa ameuacha utamaduni wa kwao na kwa hiyo ni maudhui ya usasa (UK wa 29-35).
- ❖ Katika hali sambamba, tunamwona Baba, babake Lanina akisema kuwa haelewi vijana wa siku hizi yaani wametia fora na wanataka kuwa wazungu, wanataka kuwa wanaume kwa sababu Lanina ametupa familia yake kando na anapigania usawa, ni kwa hiyo, ni kweli kusema kuwa kuna maudhui ya usasa (UK 36-42).

25. Njaa.

- ❖ Ni ukosefu wa chakula unaosabishwa na umaskini. Kuna maudhui ya njaa katika tamthilia ya *'Kilio cha haki'* kwa mfano, tunamwona Mzee Mkongwe akilalamika akisema eti wamezungukwa na njaa fisadi, uchungu wa dhiki, hasira na laana(UK 5).
- ❖ Kuongeza hapo, tunamwona Lanina anaelezea kuwa wafanya-kazi katika shamba la Delamon, hawali, hawanywi na wanakufa kwa njaa. Ni ukweli kuna maudhui ya njaa katika tamthilia ya *'Kilio cha haki'*(UK wa 25),

26. Mapinduzi/ ukombozi.

- ❖ Ni mabadiliko yanayosababishwa na siasa kwa madhumuni ya jambo fulani. Mapinduzi katika tamthilia hii yanajitokeza miongoni mwa waafrika wanaoongoza harakati za kumwondoa mzungu. Kwa mfano, tunamwona Lanina- mwanamke jasiri anaongoza siasa za kupigania haki zao ili wamfagilie mbali kaburu.
- ❖ Vile vile, Musa, Dewe na wafanya-kazi wengine wanaongoza mgomo wa kuwafukuza wazungu. Kwa mfano, Dewe anashika gongo na kumwagisha damu ili wapate uhuru. Matendo haya lazima yanadhihirisha maudhui ya mapinduzi(UK 72).

27. Uchochezi.

- ❖ Ni hali ya kufanya watu kuanza kupigana au kupigania kitu. Kwa mfano, katika tamthilia ya *'Kilio cha haki'* Lanina, Dewe na Musa wanachochea mgomo ya kupigania haki zao. Kwa mfano, UK wa 2 unamwonyesha Lanina akitiwa kizuizini na Henderson Kamishna wa polisi kwa sababu amechochea mgomo baina ya wafanya-kazi.
- ❖ Juu ya hayo, Dewe na Musa nao wanachochea mgomo wa kumkandamiza Delamon, kwa mfano, tunawaona ofisini mwake wakisema kuwa watatumia nguvu zao kuzivunja pingu walizowatia na hatimaye wanawauwa Delamon, shindo na Teleki(UK 72).

28. Matabaka /utabaka

- ❖ Ni utofauti uliopo kati ya pande mbili au zaidi kwa misingi ya kiuchumi, kielimu, kisiasa na kadhalika. Matabaka yanajitokeza kati ya watawala na watawaliwa, kwa mfano, Kamishna Henderson, Delamon ni viongozi wanaongoza nchi huku wafrika ni watawaliwa. Isitoshe, kuna matabaka baina ya makabwela (*wafanya kazi*) na mabwenyenye (*matajiri*). Kwa mfano, Bwana Delamon ni tajiri yaani ana mashamba mengi na hata ni kiongozi (*mkurugenzi*) ilhali waafrika kama vile Lanina, Baba, Mwengo, Mzee Mkongwe na wengine ni maskini wanaokufa kwa njaa.

FANI/MBINU/TAMATHALI ZA SEMI KATIKA TAMTHILIA YA KILIO CHA HAKI.

Fani ni jumla ya mbinu za kisanaa/lugha ambazo mwandishi anazitumia kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira.

Mwandishi Alamin Mazrui ametumia mbinu zifuatazo katika tamthilia yake ya *'kilio cha haki'*.

1. Takriri/mrudio.

- ❖ --Hii ni mbinu ya kurudiarudia neno, kirari, kishazi, au sentensi kwa ajili ya kusisitiza ujumbe. Kwa mfano. Musa anapozungumza na Dewe kuhusu Lanina baada ya kukamatwa na polisi anasema, *'lazima! Lazima wantie malalani!'*(UK wa 2)
- ❖ --Pia, katika UK 2, Musa anapomwambia Dewe kuwa kumtia matatani Lanina, kunaweza kuchemsha ari ya wafanya kazi wengine, Dewe anajibu ati *'ni kweli'* na Musa anaendelea kusisitiza akisema, *'Ni kweli tu! Nakwambia ni kweli. Neno 'kweli' limesisitizwa.*
- ❖ --Aidha, katika UK wa 3 Dewe anamwomba Musa ili akaendeleo na kumaliza kusoma, Musa anasema *'Ndiyo, ndiyo! We maliza tu. Enh?'*
- ❖ --Fauka, UK wa 4 unaonyesha mbinu ya takriri mwandishi anaposema, Dewe *'anatafutatafuta'* tena aliposimama.
- ❖ Vile vile, katika UK wa 6, tunamwona Musa akimwambia Dewe eti wameanza kuzaliwa wengine akisema, *'Twende ndugu! Twende....'* Neno *'twende'* ni la takriri.
- ❖ --Isitoshe, wakati Delamon anapozungumza na Zari kuhusu sauti za wafanyakazi wanaofanya migomo wakiimba, zari anasema *'Yaa.....yaani ni wale..... wale viongozi wao tu. Ni yule Laina tu....yule mwanamke mshenzi ..yule....'*
- ❖ --Juu ya takriri, wakati wafanya-kazi wanapolalamikia haki zao, *wanasema''kwa nini...eee'' 'kwa nini ...eee' (UK wa 8)*
- ❖ --Kando nahayo, katika UK wa 3, tunaona Dewe akiwalaumu makaburu kwa kuendeleza udhalimu wao, kwa mfano anasema, si *unakumbuka ile kesi ya yule msichana wa kishamba. 'Aliyetafunwa-tafunwa'na majibwa ya bwanashamba. Neno 'tafunwa' limerudiwarudiwa.*
- ❖ --Waidha, kuna takriri katika UK 9 ambapo sauti za wafanya-kazi zinasikika zikilalamika, wakisema,

'Nirudishie jasho langu!

Nirudishie damu yangu!

Nirudushie haki yangu!

Nirudishie utu wangu!

- ❖ --Fauka, tunamwona Delamon anawakaribisha Lanina na Tereki akisema, *'karibuni! Karibuni!'*(UK II)
- ❖ --Ghalibu, wakati Kachero na Shindo wanapomshawishi Tereki kuungana nao na kusema wampe muda wakufikiria, baada ya kuondoka katika UK wa 19, Shindo anasema, *'Mzungu huyu anajaribu kumsaidia na yeye ati anajidai anataka kufikiria kwanza. Kufikiria! kufikiria!Ana akili gani za kufikiri, mshenzi yule!'*
- ❖ --Vile vile, katika UK wa 21, tunamwona Kachero wa 1 *'anapekuapekua makaratasi'*.Neno *'pekua'* lazima limerudiwarudiwa.
- ❖ --Fauka ya hayo, tunamwona Mwengo akimwita mke wake akisema, *'Lanina! Lanina!'*.*'Lanina'* ameitwa mara mbili hivi ni takriri(UK29)
- ❖ --Pia, tunamwona Lanina anashika mtoto wake Dida na kumpeleka kitandani lakini Mwengo anabaki peke yake. Anakaa kochini kichwa mikononi. Halafu ghafla anainuka na kuanza *'kuzungukazukazunguka'* na kusema peke yake. Neno *'zunguka'* limetamkwa maradufu (UK 30)
- ❖ --Aidha, UK 31 unamwonyesha Mwengo amechanganyikiwa na kusema, *'simfahamu tena! Simfahamu mke wangu!'* kirai *'simfahamu'*kimerudiwarudiwa.
- ❖ --Bila shaka, tunamwona Mwengo akimhuhurumia Lanina kwa mapigo *'akimpapasapapasa'* na halafu anasema, *'Ah! Lanina pole....kwa...kwa... hamaki zangu....'* Maneno *'papasa'*na*'kwa'* yamwerudiwarudiwa(UK 31).
- ❖ --Isitoshe, tunamwona Lanina anaghairi kutilia maanani utamaduni wa kwao, kwa mfano, anasema *'utamaduni! Utamaduni! Utamaduni ni kitu gani Mwengo?'*. Neno *'utamaduni'* limekariwa(UK 32).
- ❖ --Pia, tunamwona babake Lanina anamkataa akiwa na hasira na kusema ati si mtoto wake, kwa mfano, anasema, *' Mimi! Mimi nizae mke-mume! Heee-he! Labda mtu mwingine, si mimi'*. Neno *'Mimi'* limetamkwa mara kadhaa(UK 38).
- ❖ --Waaidha, wakati mamake Lanina anapomtunza na kumfunza adabu katika uk wa 41, Lanina anajaribu kujitetea lakini Mama anasema, *'La! La! La! Lanina'*.vile vile, anaendelea kumwambia, *'mwanangu, fikira hizo za kihalifu... fikira hizo za kujifanya sawa na waume fikira hizo za kuharibu mila zetu fikra hizo Lanina umezitoa wapi?'*.Neno *'fikra'* ni la mrudio.
- ❖ --Juu ya hayo, kuna takriri katika UK wa 72 wakati ambapo Dewe anashika gongo anasema,
'Dewe: Dami imwagikeee!
Watu: Damu imwagikeee! Imwagikee!

- ❖ --Kuongeza juu ya takriri, UK wa 44 unamwonyesha Musa akivutana na mfanya-kazi ingawa wanatenganishwa na wenzao halafu MK anasema, *'mmemwona! Mmemwona alivyonirukia! Kichaa huyu!'*

2.Kejeli

- ❖ --Ni mbinu ya matumizi ya maneno yenye dharau. Pia, maneno yanayotumiwa yanakera. Kwa mfano, Musa anatumia kejeli katika UK wa 2, anaposema, *'wanastahili kuuwa wale! Panya wanyonya watu'*.
- ❖ --Aidha, katika UK wa 2, Musa anawaita *'mafisi'* wazungu kwa sababu wamemtia Lanina kizuizini.
- ❖ --Vile vile, Musa anaendelea katika UK wa 4, akitumia kejeli zake kama vile, *'kwa nini iheshimiwe! Shenzi!'*
- ❖ --Waidha, wakati Dewe anapomsomea akisema kuwa, Lanina amekamatwa kwa kuchochea mgomo wa kikatili, Musa anakejeli kwa kusema, *'Hapo hapo tu ! Ati kashochea mgomo wa kikatili. Wapumbavu wale'(UK 3).*
- ❖ --Aidha, UK wa 14, unaonyesha kejeli za Askari 1 Lanina anaposema eti anapigania na kutetea haki zao, Askari anasema, *'.... Mpumbavu wee!'*
- ❖ --Bila shaka, mbinu ya kejeli inaonekana katika UK 37 Lanina anapomsalamia babake, Baba anasema, ati asimsalamie, akisema, *'Babako mimi, mimi sikuzaa Malaya!'*. Anaendelea katika UK 38 akimwita binti ya shetani, katika UK 42, Lanina anaitwa mwanaharamu. Maneno haya yote yanaonyesha mbinu ya kejeli.
- ❖ --Waidha, migogoro baina ya wafanya-kazi katika UK wa 43-48 inaonyesha kejeli. Kwa mfano, Musa anamwita mfanya-kazi mjinga akisema, *'mjinga!Tena mjinga sana!'* Aidha, Mk naye anatumia kejeli katika UK 44, anaposema kuwa Musa ana wazimu, anasema ati Musa ni kichaa.
- ❖ --Isitoshe, Bwana Delamon naye anatumia maneno ya kejeli katika UK 66, kwa mfano, anasema, *'Huyu mwanamke ni punda, hana fadhili'*

3.Utohozi.

- ❖ --Ni mbinu ya kuswahilisha maneno yasiyo ya Kiswahili yatamkike kama ya Kiswahili, mathalani, mwandishi ametumia mbinu ya utohozi katika UK 44, kwa mfano, 'Dewe anamwendea MK na kumshika *'mashati'*. 'Shati' ni neno la utohozi kutoka *'Shirt'* la Kiingereza.
- ❖ --Pia, Musa ametumia neno la utohozi akilalamikia jinsi wanavyofanya kazi bila kupumzika yaani anasema *'sisi binadamu ala! Si machine'*. Neno *'machine'* limetoholewa kutoka neno *'machine'* la Kiingereza(UK 45).

- ❖ --Waidha, neno *'polisi'* kutoka neno *'police'* la Kiingereza limetumiwa kama utohozi (UK 2, 15)
- ❖ --Isitoshe, neno *'Kamishna'* kutoka neno la Kiingereza *'commissioner'* linaonyesha utohozi (UK 2).
- ❖ --Aidha, neno *'kesi'* kutoka neno la Kiingereza *'case'* limetoholewa (UK 3).
- ❖ --Vile vile, mwandishi ametohoa neno *'kidemokrasia'* kutoka neno *'democracy'* la Kiingereza (UK 15).
- ❖ --Hatimaye, kuna maneno ya utohozi katika UK 21, kwa mfano, *'paketi'* kutoka neno *'packet'* la Kiingereza, *'wiki'* kutoka neno *'week'* la Kiingereza.

4. Methali.

Ni mbinu ya Sanaa/kifasihi inayotumia mafumbo. Kwa ufupi, methali ni kifungu cha maneno ya hekima yenye maana fiche. Uboru wa hekima hiyo hutegemea muktadha ambako methali hiyo imetumika. Mwandishi wa tamthilia ya *'Kilio cha haki'* ametumia methali kama vile; *'Mwenye nguvu mpishe'* Musa anapodharau sheria za makaburu akimaanisha kuwa *'wenye mamlaka huamua'* (UK wa 4)

- ❖ --Methali kadhalika imetumiwa na mamake Lanina akijaribu kumponya matusi na kejeli za babake kwa sababu amejiumba katika harakati za kupigania haki. Kwa mfano, anasema, *'midomo ya waja haikosi kusema, na kizuri hakiwachi kutiwa ila!'* .Baba naye anamjibu, *'Dalili ya mvua ni mawingu'* kwa maana *'cheche za maneno yanayosemwa kwa Lanina lazima yaweza yakazua ukweli'* (UK 35)
- ❖ --Aidha, Mama ametumia methali ya *'mkosa chema hawachi -- kuguna'* akimaanisha kuwa *'watu wanamsema na kumwonea kijicho mtotowe Lanina kwa sababu amepata kazi mjini nao wameshindwa'* (UK 37)
- ❖ --Pia, wakati Tereki, Matovu na Pelekha wanapomdadisi Lanina kukubaliana na Delamon, Matovu anamwambia Lanina kupoa moto akimkumbusha methali ya *'hasira hasara'* kwa maana ya kwamba hasira ya Lanina yaweza kuzusha madhara hasi (UK 52).
- ❖ --Juu ya hayo, kuna methali ambayo imetumiwa na wakili akijaribu kumwambia Lanina eti ajiepushe na mambo ya kupigania haki. Kwa mfano, anasema, *'siasa nini mchezo mchafu'* kwa maana hali za siasa zinaweza kumharibu maisha yake UK 76

5. Tanakali sauti

Ni tamathali ya semi ambayo ambayo mhusika anauliza swali huku akijua jibu lake . Kwa mfano, katika UK 25, Kachero wa 1 anagusa na kumpapasa Lanina, Lanina anamwita mhuni lakini Kacwero wa 1 anaendelea kumwuliza, *'uhuni? Wewe*

unaniita mimi mhuni? Maswali haya ni ya tashtiti kwa sababu Kachero1 anajijua eti ameitwa *mhuni*.

- ❖ --Aidha, tunaona Pelekha anamwambia Matovu kuedelea na maneno ya kuanza kumshawishi Lanina lakini Matovu anaendelea na kuuliza swali kama vile, *'mimi?'* Swali hili ni la tashtiti yaani Matovu anajua eti Pelekha amekuwa anasema yeye.

6. Mseto/ kuchanganya ndimi

- ❖ --Ni mbinu ambayo lugha za kigeni zinatumiwa katika maneno au sentensi za Kiswahili. Kwa mfano, Delamon anamwita Kimbo, Kimbo anajibu *'yes-saaa! Comin-saa'* badala ya kusema *'naam, ninakuja Bwana'*(UK 9).
- ❖ --Aidha, katika UK10, tunamwona Delamon kwa hasira akiwatusu Kimbo, Shindo na Zari kwa mfano, anawaita *'foolish baboons'* badala ya *'nyani wapumbavu'*.
- ❖ --Vile vile, kuna mseto katika UK wa 45, kwa mfano, Tereki anasema, *'Ndiyo, kweli hatulipwi overtime....'* Badala ya kusema *muda wa ziada*.

7. Ushairi.

Shairi ni maandishi/wimbo unaoelea wazo/ mawazo au hisia juu ya maisha.

- ❖ --Pia, ushairi ni tukio, hali au wazo ambalo linaonyeshwa kwa upangaji mzuri wa maneno. Kwa mfano, kuna matumizi ya shairi yaani,

'Nirudishie jasho langu!

Nirudishe damu yangu !

Nirudishe haki yangu!

Nirudishie utu wangu!

- ❖ Hili ni shairi ambalo limeundwa kwa ubeti mmoja, mistari minne, kipande kimoja na vina vya mwisho vinavyofanana toka mwanzoni hadi mwishoni (UK 9)

8. Nidaa.

Ni tamathali ya semi ambayo inaonyesha kushangaa au kushangazwa na jambo fulani. Alama za mshangao zinatumiwa. Kwa mfano;

- ❖ --Dewe- eee! Uk 1

- ❖ *Hee! Musa! Musa! Sikiliza!*

- ❖ *Sikiliza habari hizi !*

- ❖ *Habari za Lanina!*

- ❖ *Sikiliza eh!* anatega masikio kwa hamu naye anasema, *'lete Dewe! Soma Bwana! Soma'*.

- ❖ --Aidha, katika, Dewe anasoma habari inayoshangaza kwa kusema eti Lanina atapelekwa mahakamani, na hapo Musa anashangaa na kusema, *'unaona! Unawaona hawa Dewe! Lo! Lo! Lo! Ati Lanina ameshiriki katika mauaji !'*(UK 3).

- ❖ --Eh-he! Uk 4
- ❖ --Musa anasema, 'Lo! kweli kabisa Dewe!' UK9 anasema, 'Halo ! Kamishna.....ooo nzuri tu.....Ha!
- ❖ Ha! Ha!....'
- ❖ --UK wa 9, Delamon anapoita Kimbo anasema, 'Kimbo!' 'Kimbooo!'
- ❖ --Uk wa 10-11 Delamon anashangazwa na sauti za wafanya- kazi anasema, 'Eee mola wangu! Balaa gani hii!'
- ❖ --Kachero wa 2 anashangazwa na maneno ya Lanina na anasema, 'La! La! La! Umekosa Lanina!' UK22.
- ❖ --UK 25 Kachero wa 1 anashangazwa na Lanina ambaye amemwita mhuni na anasema, 'uhuni? Wewe unaniita mimi mhuni? !'
- ❖ --UK 31, Mwengo anachanganyikwa na mienendo ya Lanina na kusema, 'Lanina! Kumbe...kumbe wamekutesa huko!'
- ❖ --Mamake Lanina anashangazwa na maneno ya Baba (*mumewe*) anaposema, 'mwanao! Sema mwanao!' na Mama anasema, 'Ewe mola!....'.
- ❖ --Uk 32 Mwengo anapomwambia kufuata utamaduni wao, Lanina anashangaa kusikia hayo na kusema, 'utamaduni ! Utamaduni! Utamaduni ni kitu gani Mwengo!' N.K

9. Taswira/ jazanda

Ni mkusanyiko wa picha zinazoundwa na maelezo ya msanii katika kazi yake ya ubunifu. Taswira hujengwa kutokana na matumizi ya tamathali za semi hasa sitiari, na tashbihi.

- ❖ --Maneno ya Musa yanajenga taswira/ picha ya njaa kwa mfano, anasema kuwa wameanza kuishi kinyama, wanashindana na mbwa na mapaka waking'ang'ania makombo yaliyotupwa mapipani na watu UK 1.
- ❖ --Aidha, kuna picha ya umaskini inayojegwa akilini mwa msomaji baada ya kusikia eti nyumba ya Mwengo ina chumba kidogo, chenye kochi moja bovubovu, ndani mna viti viwili vidogo, masigiri mawili na visahani UK 29.
- ❖ --Pia, nyumba ya wazazi wake Lanina nayo inajenga picha ya umaskini yaani wanalala katika kibanda (UK 36).
- ❖ --Waidha, maneno ya babake Lanina yanajenga picha ya ukali wake. Kwa mfano, anamwita Lanina Malaya, anamwita binti ya shetani, anamwita msaliti. Kuongeza hapo, anasema 'Mimi ndiye simba wa nyumba hii. Ningurumapo sitaki kusikia Lakini zenu za kijinga hapa' Maneno haya Lazima yanajenga taswira ya ukali akilini mwa msomaji.

10. Tasfida.

- ❖ --Ni tamathali ya semi ambayo kwayo maneno yatumikayo yanapunguza ukali, aibu na kero za msemaji. Pengine, mbinu hii inajumuisha maneno yatoayo heshima. Kwa mfano, Delamon anapewa heshima kwa kuitwa ‘*Bwana*’ UK2. Aidha, Mkongwe anapewa hesimakwa kuitwa ‘*Mzee*’ UK5. Vile vile Ingeli naye anapewa heshima kwa kuitwa ‘*mzee*’UK 5.
- ❖ --Hali kadhalika, mwandishi anatumia tasfida kusafisha aibu. Kwa mfano, wakati Askari anapojaribu kumfanyia Lanina mabaya kwa kujaribu kumbusu na kumpasulia nguo, anasema, ***Lanina anampiga goti kwenye sehemu zake za chini*** Sehemu hizo zimefichwa kutamkwa wazi UK 73.

11. Tashbihi/ Mishabaha.

- ❖ --Ni tamathali ya semi ambayo vitu viwili au zaidi vyenye sifa tofauti hulinganishwa kwa kutumia viunganishi kama ***vile, mithili ya, kama, kama kwambia ‘mfano wa , fanana na*** N.K. Kwa mfano;Katika malalamiko ya wafanya-kazi wakijaribu kusawiri vilio vyao, tunasikia sauti zikisema, *mimi niliyekuwa nikiteswa kama fahali*. Neno ‘*kama*’ limetumiwa kulinganisha hali ya fahali na wafanya kazi (UK7)
- ❖ --Aidha, Kachero wa 1 katika maneno yake akimwambia Lanina kuwa yeye na wenzake hawatosheki anasema, ‘*nyinyi ni kama punda msiojua fadhila*’UK 22.
- ❖ --Waidha, Mzee Ingeli naye anatumia tashbihi anaposhukuru mjukuu wake kwa wimbo nyororo anasema,‘*kazi imekuwa kama hatia ya mauti*’(UK56) Anandelea kusema, ‘*kunyanyaswa kunatufuata kama mkia*’.

12. Uzungumizi nafsia / uzungumzaji nafsia

- ❖ --Ni matumizi ya lugha ambayo mhusika anazungumza peke yake. Kwa mfano, tunamwona mhusika Mwengo anazungumza peke yake baada ya Lanina kuondoka na kumpeleka kitandani mtoto wake. Mwengo anajisemea, ‘*simfahamu tena Lanina. Kila uchao anazidi kubadilika....*’. Maneno haya na mengine yanahakikisha mbinu ya uzungumzaji nafsia (UK 30).
- ❖ --Aidha, mwishoni mwa kitabu (*tamthilia*) tunamwona mhusika Lanina anazungumza peke yake akisema. ‘*Hapana! Haliwezekani! Itakuwa vipi? Itakuwaje....?*’

13. Nahau/Semi

- ❖ --Ni mafungu ya maneno yenye maana fiche au isiyo wazi ambayo hutumiwa na mwandishi ili kuweka maadili katika matamshi kwa mfano, mwandishi ametumia nahau yaani Musa baada ya kusikia ati Lanina ametiwa kizuizini kwa sababu ya kuchochea mgomo,

- ❖ *'anatema mate kwa hasira' maana "anaonyesha kuudhika na tendo hilo' UK 3.*
- ❖ --Isitoshe, baada ya Delamon kuzisikia sauti za wafanya-kazi wanaolalamika anasema *"Lo! Sikilizeni sauti zao.... Zinatia hofu..."* akimaanisha kuwa sauti zao zinaogofya sana (UK 7)
- ❖ --Lanina naye ametumia nahau ya *'tilia nguvu uongo'* akimaanisha kuwa Tereki anashabiki sana uongo wa Delamon (UK 13).
- ❖ --Vile vile, Tereki anapoulizwa akiwa ameshakubali kuungana na Delamon, anatumia semi na kusema, *'haya si mambo ambayo mtu anaweza kuyakatia shauri mara moja'*. *'Katilia shauri'* ni nahau yenye maana ya *'kuamua'* (UK 18)
- ❖ --Fauka ya hayo, Baba babake Lanina naye ametumia nahau akilalamikia vijana, anasema, *'...wao ndio waliotia fora' Tia fora ni nahau yenye maana ya 'kuharibika'* (UK 36).
- ❖ --Bila shaka, Mama mamake Lanina naye ametumia nahau akijaribu kumtetea mwanake Lanina. Kwa Mfano, anasema, *'Lanina sasa ana kazi mjini, watu lazima watamwonea kijicho'.* *'Onea kijicho'* ni semi inayomaanisha kufitini (UK 37)
- ❖ --Hali kadhalika, mwandishi ametumia nahau anapoonyesha kuwa Lanina anaigia kutoka gerezani na mamake anamwona na *'kuangua kilio'*. *Kuangua kilio* ni nahau inayomaanisha kuanza kulia UK 37.
- ❖ --Mzee Ingeli naye anatumia nahau katika kioski yake akijaribu kumtetea mjukuu wake Lanina na kusema, *'Tena nisimwone mtu yeyote akimgusa mjukuu wangu au atakiona cha mtema kuni' 'ona cha mtema kuni'* ni nahau inayomaanisha kuwa *'wataadhibika wakimsumbua Lanina'* (UK 57).
- ❖ --Aidha, katika mivutano MK anawasumbua wafanya-kazi wenzake, na Dewe anatumia nahau akisema, *'usimtie maanani' akiwa na maana ya kuwa, Musa ampuuze MK'* (UK 45).

14 Sitiari /istiara

- ❖ --Ni mbinu ya kulinganisha vitu viwili au zaidi bila kutumia viunganishi. Kwa mfano, *makaburi kwa sababu ya kuwa na tamaa nyingi ni wanyonyaji, Musa anawaita mafisi.* Kwa mfano, anasema, *'.....watauona moto ukimiminika, Mafisi wale'* UK 2.
- ❖ --Aidha, anaendelea na kusema *'wanastahili kuuawa wale! Panya wanyonya damu'*.
- ❖ --Vile vile, baada ya Shindo kushindwa kuelewa matendo ya wazungu, anasema, *'nakwambia Mzungu, Bwana, bwana, mchawi kweli kweli'* Mzungu analinganishwa na mchawi (UK 15)

- ❖ --Isitoshe, Baba bake Lanina analinganisha mtoto wake na punda, , kwa mfano anasema, ‘...huyu ni punda. Kwa mfano anasema.‘.....huyu ni punda...’ akimaanisha eti *hatosheki UK 38*.
- ❖ --Fauka ya hayo, Baba anaendelea kujiita simba akiwa na maana ya kwamba ndiye anayeweza kutoa uamuzi. Kwa mfano, anasema‘*Mimi ndiye simba wa nyumba hii*’ Baba anajilinganisha na Simba yaani *asemapo, hakuna mwingine wa kusema (UK 38)*

15. Chuku/udamisi.

- ❖ --Ni fani ambayo inatumiwa na mwandishi kutia chumvi katika mazungumzo. Kwa mfano, Musa baada ya kukamatwa kwa Lanina, anasema, ‘*Lanina ameichemsha ari ya wafanya-kazi wote sasa. Lakini hawafahamu kwamba kumtia kizuizini, wafanya-kazi watazidi kuchemka, nao watauona mtoto ukimiminika (angesema wafanya-kazi watakera zaidi, na watauona moto ukienea) UK2*.
- ❖ --Aidha, maneno ya Mama mamake Lanina nayo yanatia chuku, kwa mfano, anasema, ‘*Ah! Mwanangu. Kukonda huko kukokonda macho yamekukoboka, ngozi imepapurika, umebaki mifupamitupa! Mitupu!*’ Hii ni chuku kwani Lanina akiwa amebaki mifupa mitupu, asingetebea UK 39.

16. Tashihishi/uhaishaji.

- ❖ --Ni mbinu ya lugha ambayo kitu kisichokuwa na uhai hupewa sifa za kiumbe mwenye hai. Mbinu hii inaonekana katika tamthilia ya ‘*Kilio cha haki*’ . Kwa mfano, Dewe anamwuliza Musa akisema, ‘*ungependa kurudi nyumbani kwenye mauti yanayokusubiki?*’. ‘*Mauti*’ yamepewa sifa ya binadamu ya kuweza kusubiri (UK 1)
- ❖ --Ghalibu, Lanina anatumia uhaishaji katika maneno yake, kama vile, ‘*Najichekea...kwani najua vyema kwamba sijaizoea hiyo hali njema ijitembezayo kwa shairi na ngoma*’ Kwa kweli hali haiwezi kutembea na kwa hiyo ipepewa sifa za kiumbe mwenye uhai (UK 34).
- ❖ --Bila shaka, mwandishi anatuonyesha mbinu ya uhaishaji wakati Delamon anapocheka. Mathalani, anasema, ‘*Anaendelea kucheka, kila mmoja anamtazama. Kicheko chake kinakufa polepole...*’ Hii ni mbinu ya uhaishaji kwa sababu ‘*kicheko*’ kinaweza ‘*kufifia polepole lakini hakiwezi kufa (UK 72)*.

17. Maswali ya balagha.

- ❖ --Haya ni maswali yasiyohitaji majibu. Hapa mbusika anaweza kuwa anasema peke yake huku akijiuliza maswali kwa vile hakuna mhusika wa kumjibu. Kwa mfano, Dewe anasema peke yake baada ya MK, Pelekha na Tereki kuondoka

yaani, *'Ewe Mungu wangu we! Ni kweli haya niliyoyaona? Ni kweli haya niliyoyasikia?'* Maswali haya ni ya balagha kwa kuwa hakuna awezaye kumjibu Dewe (UK 48).

- ❖ --Aidha, maswali yanayoulizwa na Lanina mwishoni mwa kitabu ni ya balagha kwani anasema peke yake na kujiuliza, *'.... Itakuwa vipi? Itakuwaje?...' (UK 77).*
- ❖ --Vile vile, baada ya Baba kumnyamazisha mkewe, anauliza maswali ya balagha mfululizo, kwa mfano. *'Nyamazaaa!! Mawaidha? Mawaidha ya shetani gani? Baada ya kutonitii sasa mnajaribu kunihadaa?'* Maswali haya yote ni ya balagha kwa sababu mtu ambaye angemjibu amenyamazishwa (UK 42).

18. Aklonimu.

- ❖ --Ni mtindo wa lugha ambao unajihusisha na matumizi ya vifupisho. Kwa mfano, herufi ya kwanza ya neno / jina inaunganishwa na herufi ya neon/jina jingine kuwakilisha neno kamili. Kwa mfano, mwandishi wa *'Kilio cha haki 'ametumia MK kuwalikisha Mfanya- kazi (UK 43)*

19. Alama za dukuduku/mdokezo

Ni mbinu ya kifani au kisanaa ambayo kwayo mtu husema baadhi ya maneno na kuacha mengine Hali hii inasababishwa na, kilio, hasira, kicheko, furaha, mchanganyiko na mazungumzo ya simu, hofu, au mtu kukatisha maneno kwa mfano,

- ❖ --Zari anapoambiwa na Delamon kusikiliza sauti za wafanya kazi, zari anayetema na kusema, *'Ni....ni.... ni watu wachache... niwaachache tu Bwana Delamon. Nadhani....'* (UK 8).
- ❖ --Aidha, Zari anaendelea na kusema *'Yaani....yaani ni wale...waleviongozi wao tu. Ni yule Lanina tu.... Yule mwanamke mshenziyule....'* (UK8)
- ❖ --Mazungumzo baina ya Delamon na Kamishna Henderson nayo yanadhihirisha mdokezo. Kwa mfano, *'Halo! Kamishna ooo nzuri tu... Ha! Ha! Ha!...'* UK 9
- ❖ --Delamon naye anachanganyikiwa na sauti za wafanya-kazi na kuambia Kimbo kuwaita Lanina na Tereki, *'nenda kamwite...aaa....aaa....'* (UK 10)
- ❖ --Zari pia anadokeza maneno yake kwa sababu ya hasira akitaka kuwatusu tereki na Lanina ingawa anakemewa na Delamon. Kwa mfano, *Nyinyi ndio washenzi mnao... mnao...'* (UK 12).
- ❖ --Mdokezo kadhalika unanekana wakati Mwengo anapojaribu kumtuliza Lanina kwa mapigo ya makaburu anasema, *'Ala! Lanina pole.....kwa....kwa hamaki zangu'* (UK 31)

- ❖ --Isitoshe, Mwengo anapomwambia eti Lanina ameipuuza familia yake na ndiye anayewapikia watoto, anasema, *Mimi... mimi ni mume wako nimekuwa kama... kama aah!.....kama si mume tena*' (UK 32).
- ❖ --Naye mamake Lanina kwa sababu ya kuchanganyikiwa na maneno ya watu, anadokeza maneno akijaribu kumwambia mtotowe. Kwa mfano, *'Lanina....Mwengo alikuja hapa....akatwambia kuwa watu...watu.... Wanasema ati wewe nini....'*(UK 40)

20. Nyimbo.

- ❖ --Ni matumizi ya sauti zenye toni ya mahadhi ama ya juu au chini. Kwa mfano, Lanina anaimba wimbo wa kupigania haki ambao unafurahisha mwajiri wake Ingeli (UK 56)
- ❖ --Pia, wafanya-kazi waliogoma sauti zao zinajitokeza zikiimba nyimbo za siasa (UK 66), UK 7).
- ❖ --Lanina pia anafahamisha Kachero wa 1 akisema, *'Nyimbo zetu zilikuwa zinadhihirisha udhalimu tunaofanyiwa na Delamon...'* (UK 23)
- ❖ --Ni mbinu ambayo sauti zitolewaza huiga milio, na sauti za vitu. Kwa mfano, Lanina anaonekana nyumbani akiwa amelala kisha anausikia mlango unagongwa *'ko! Ko! Ko!'* (UK 49).

21. Majazi/ Majina ya Lakabu.

- ❖ --Ni upaji wa mhusika jina kulingana na kazi yake, tabia yake, maneno yake, umri wake, mavazi yake pamoja na matendo yake, Kwa mfano. Mkongwe amebandikwa jina hilo kwa sababu ni mtu mkuu kabisa (UK 5), Pia Mfanya-kazi (MK) amepewa jina hilo kwa sababu anafanya kazi katika shamba la Delamon (UK 43). Aidha, Makachero (*Kachero wa 1 na wa 2*) wamepewa majina hayo kwa sababu wanamjulisha Delamon mambo yanavyoendelea.

22. Dhihaka.

- ❖ --Ni tamathali ambayo kwayo mtu kwa makusudi husema maneno kumbeza mtu mwingine. Dhihaka ni tofauti kidogo na kejeli kwa sababu maneno ya dhihaka yanasemwa kimzaha. Kwa mfano, Lanina akiwa gerezani, Askari anaingia na kumsalimia huku akichekacheka, mathalani, anasema, *' Je dada! Habari ?'* Anamwuliza habari kimzaha akijua eti ni mbaya (UK 73).

23.Taharuki .

- ❖ --Ni mbinu ya kumwacha msomaji na hamu au mvuto ya kuendelea kusoma ili ane yanayofuata. Kwa mfano, msomaji afikapo Dewe anapokamata gongo na kuuliza ikiwa damu imwagike, bila shaka atakuwa na hamu ya kuendelea kusoma (UK 72).

- ❖ --Vile vile, mwishoni mwa tamthilia tunamwona Lanina katika bahari ya mawazo akimwambia mamake kuwa atazipenya kuta za matofali na atoroke arudi nyumbani lakini hatujajua ikiwa Lazima ameenda nyumbani, hiyo bila shaka ni taharuki (UK 77)

HULKA/WASIFU/UTENDAJI/SIFA ZA WAHUSIKA KATIKA TAMTHILIA YA KILIO CHA HAKI

Sifa ni jinsi mhusika anavyosawiriwa kwa kuregelea utendaji wake.

1. Bw. Delamon

--Ni mnyonyaji. Unyonyaji ni hali ya mtu kupata mapato makubwa akitumia nguvu za wafanya-kazi wengine kama vile kuwapatia mishahara mdogo. Kwa mfano, Delamon anafanyisha wafanya-kazi wengi lakini anawapatia mishahara duni. Kwa mfano, tunamwona Lanina anawaambia kuwa makaburu wamekuja kuinyonya nchi yao (UK 13)

--Ni tajiri. Tajiri ni mtu mwenye mali na pesa za kutosha. Kwa mfano, Delamon ana mashamba mengi na ana wafanya-kazi wakiafrika waliojiriwa (UK 1)

--Aidha, ni katili. Katili ni yule anayetendea wengine kinyama bila kujali maisha ya yao. Kwa mfano, tunamwona anapeleka Lanina jelani kwa sababu amechochea mgomo wa kupigania haki zao. Aidha, tunamwona ananyima wafanya-kazi wake mishahara minono.

--Vile vile, ni mkarimu kwa mfano, tunamwona anaambia Kimbo kuita Tereki na Lanina, baada yao kufika anawaribisha yaaani anawapa mikono, na kuwaongoza hadi vitini. Aidha, ndiye anayewavutia viti na anataka kuwaletea chai ingawa wanaikataa (UK -12)

--Isitoshe, ni mbaguzi. Mbaguzi ni yule mtu anayependelea upande mmoja na kuuacha mwingine kihadhi, kisiasa kiajira, kirangi, kielimu, kikabila na kadhalika. Kwa mfano, tunamwona anawabagua wafanya-kazi wake kama vile, Matovu, Pelekha, Kimbo, Wakili na wengine anawapenda sana kuliko Lanina, Dewe Musa na waafrika wengine.

--Ni kiongozi ambaye ana mamlaka kwa waafrika. Kwa mfano, tunamwona ofisini akifanya-kazi zake kama Mkurugenzi (UK 7)

--Ni mnyanyasaji/mwenye dhuluma. Ni yule anayetesa watu bila huruma. Kwa mfano, tunamwona anapigia kamishna mkuu wa polisi kuwa wamechochea mgomo wa kupigania haki zao. Aidha, anawanyanyasa wafanya-kazi wake kwa kuwanyima malipo ya 'overtime' ingawa wanafanya kazi kwa muda wa ziada (UK 45)

--Ni mwenye kujifanya/mkaidi. Delamon ana tabasamu ya fisi mwenye njaa. Kwa mfano, tunamwona anawaita Lanina na Tereki rafiki zake ingawa mwishoni mwa onyesho la 1, anawapeleka gerezani (UK 11-14)

--Hali kadhalika, Delamon ni mwenye ubinafsi. Anapenda kujitosheza na kujipatia hali nzuri bila kuwaangalia wengine. Kwa mfano, tunamwona akisema, '*...watu wote hawawezi kuwa sawa duniani ! Hawawezi kupata mshahara kama ninaopata mimi*'(UK 66)

--Ni mvutaji sigara. Uvutaji sigara ni hali ya kuvuta sigara. Kwa mfano, tunamwona anatoa kiko chake anajaribu kukiwasha lakini kinamshinda (UK 10).

--Delamon ni mwoga, kwa mfano, tunamwona amechanganyikiwa sana baada ya wafanya-kazi kugoma na punde anaamua kumpigia Henerson Kamishna wa polisi. Aidha, tunaona anasema eti sauti zao zinatia hofu (UK 7-9)

--Hatimaye, ni mwenye hasira ya karibu. Kwa mfano, tunamwona anakasirika kwa sababu YA malamiko ya wafanya- kazi na anawafokea Shindo na Zari (UK 7)

2. Lanina

Ni mkewe Mwengo. Ni mwanao Baba na Mama. Lanina ana sifa zifuatazo;

--Kwanza, Lanina ni mchochezi wa mgomo. Kwa mfano, tunamwona anaongoza wafanya-kazi kugoma, tunamwona anatiwa kizuizini na Mkuu wa polisi Kanishna Henderson kwa sababu ya kuchochea ngomo (UK 20)

--Aidha, Lanina ni mvumilivu. Kwa mfano, tunamwona anakabiliwa na hali ngumu lakini anaivumilia. Kwa mfano, anateswa na Delamon kwa kutiwa nguvuni, anapigwa makofi na kuvutwa masikio na Kachero wa 1, anasumbuliwa kimapenzi na Askari ambaye anataka kumbaka lakini haya yote anayavumilia.

--Waaidha, Lanina ni shujaa. Shujaa ni yule anayetenda bila kuogopa kwa hali ile yoyote. Kwa mfano, tunamwona hamwogopi Delamon anamwambia kwa imara kwamba, Makaburu hawakuja kunufaisha waafrika bali wamekuja kuinyonya nchi yao (UK 13).

--Hali kadhalika, Lanina ni mwenye kutia bidii kazini kwa mfano, tunamwona anafanya kazi ya biashara katika kioski ya Mzee Ingeli ya kuuza uji na chai baada ya kufukuzwa na Delamon. Kwa mfano, tunamwona anawapa wateja uji (onyesho la 8).

--Vile vile, Lanina anaonyeshwa kama mwenye mapenzi. Kwa mfano, anapenda Mamake yaani tunamwona akisema, '*mpenzi mama, nitarudi nyumbani. Nitarudi hata kama ni kifoni....*' Bila shaka, maneno haya yanaonyesha mapenzi (UK 77).

--Lanina anaipenda familia yake kwa mfano, tunamwona anamkumbatia mtoto wake Dida. --Aidha, tunamwona baada ya kutiwa kuzuizini, anasema kwamba wakili aijulishe familia yake (UK 76)

--Juu ya hayo, Lanina ni mwenye msimamo thabiti yaani anayasisitiza yale anayoyasema. Kwa mfano, tunamwona amejitoa mhanga kupigania haki za wafanya-kazi wenzake, yaani tunamwona wakili akimwambia eti siasa ni mchezo mchafu auachie wanaume lakini Lanina anamjibu kwa uthabiti kuwa ikiwa siasa ni mchezo mchafu lazima usafishwe (UK 76).

--Pia, Lazina ni mvutaji sigara. Tunamwona baada ya kufika nyumbani akitoka gerezani anatoa paketi ya sigara na kuchukua moja anaiwasha. UK 31). Pia, tunamwona anatoa sigara nyingine na kuiwasha. Anaivuta kwa nguvu na kutoa moshi mwingi huku akiutazama unavyopaa hewani (UK 33)

--Ghalibu ya hayo, Lanina ni mzalendo. Ni yule anayependa nchi yake na kuwa tayari kuipigania na kuifia. Kwa mfano, anaongoza mgomo wa kupiganira haki za wafanya-kazi na tunamwona anatiwa kizuini (UK 2). Mathalani, tunamwona anasema kuwa mgomo uliofanywa na wafanya-kazi haukuwa halifu (UK 21) Hali kadhalika, tunamwona akisema eti Delamon ndiye Bwana, wao ni watumwa katika nchi yao

--Fauka ya hayo, ni mpenda umoja. Ni yule ambaye anajali masilahi ya watu wote bila kujibinafsisha na mambo. Kwa mfano, tunamwona Kachero wa 2 akimwambia juu ya ubnafsi, Lanina anasema, '*La! Ama tupate sote au tukose sote*' UK 26. Aidha, tunamwona anamwambia Delamon kuwa mjadala wowote juu ya malalamiko yao ni lazima ufanywe na watu waliowakilisha (UK 12).

--Bila shaka, Lanina ni mpiganiaji haki. Ni yule ambaye anang'ang'ania haki itendeke ipasavyo. Tunamwona anaambia Askari kweli baada ya kushtakiwa kwa hatia ya kuchochea mgomo kwamba wanajaribu kutetea haki zao tu (UK 14).

--Isitoshe, tunamwona anamwambia Mwengo kuwa naye ni mfanya-kazi na anajua taabu zao zote za kudhulumiwa, na kuyaondoa au kayakomesha mambo hayo ni lazima wapiganie haki zao na kuwa na msimamo thabiti (UK 31).

--Isitoshe, Lanina ni mpenda usasa, kwa mfano, anapigania usawa wa kijinsia yaani anataka kujisawazisha na Mwengo mumewe. Mathalani, tunamwona akisema, '*... Sitauacha, katu sitauacha utamaduni (ukale) utilie sing'enge ukweli wa maisha yangu na ukweli wa binadamu wangu*' (UK 33)

--Sifa kadhalika, Lanina ni mkaidi. Kwa mfano, anapuuza majukumu yake kimakusudi eti anataka mumewe Mwengo ajipikie chakula, alee watoto. Mathalani, tunamwona Mwengo analalamika akisema eti ameanza kujipikia mwenywewe. Kwa

mfano, tunamwona Lanina akisema, *'nikichelewa kutoka kazini basi hupika yeye'* (UK 41)

--Kwa uhakika, Lanina ni mkombozi. Mkombozi ni mtu anayesababisha watu wengine kutenda jambo la kujikomboa. Kwa mfano, Lanina anaambia wafanya-kazi wenzake ati wajitoe usingizini wapige vita vya kuondoa uongozi mbaya wa makaburu, udhalimu, unyanyasaji na unyimwaji haki.

--Hatimaye, Lanina ni mwimbaji ambaye anaimba nyimbo za mapinduzi au ukombozi UK 56.

3.Dewe.

--Kwanza kabisa Dewe ni mchochezi wa migomo. Kwa mfano, anajiunga pamoja na Musa kuamsha ari za wafanya- kazi wengine kugoma. Kwa mfano, tunamwona anaambia Musa eti warudi nyumbani kichinichini na waanze kuamsha wafanya- kazi wenzao kuendeleza kazi ya Lanina (UK 6).

--Pia, Dewe ni mfanya-kazi hodari, kwa mfano, tunamwona anafanya-kazi katika shamba la Delamon. Mathalani, tunamwona amevaa mazazi yake ya kazi na wenzake yaani Tereki, Matovu, MK, na Musa wakati wa mapumziko (UK 43)

--Vile vile, ni mpiganiaji haki. Kwa mfano, anajiuga na Musa, Lanina na wafanya-kazi wengine kuchochea mgomo ambao unasababisha mauaji ya watu watatu yaani Khindo Tereki na Delamon wakijaribu kupigania haki zao Mathalani tunamwona anashika gongo (UK 72).

--Vile vile, Dewe ni mwenye msimamo imara. Yaani, hawezi kushawishwi kuisaliti nchi yake. Mathalani, tunawaona Matovu, Pelekha na MK wakiwashawishi yeye na Musa eti wamepewa nyongeza lakini yeye anasema kwamba wanastahili kumtetea Lanina ambaye amefukuzwa kazini (UK 45).

--Hali kadhalika, Dewe ni shujaa yaani anayatenda matendo bila ya woga wowote. Kwa mfano, tunamwona anatetea haki zake kishujaa mathalani, anaonekana akishika gongo na kumwendea Delamon, Shindo na Tereki na kumwaga damu (UK 72).

4. Musa.

--Kwanza, Musa ni mwepesi wa kukasirika yaani ana hasira ya karibu. Kwa mfano, wakati Dewe anapomsomea eti Lanina ametiwa kizuizini na Kamishna mkuu wa polisi, Bwana Henderson, Musa analipuka kwa hasira na kusema, *'wanastahili kuuawa wale! Panya wanyonya watu'*(UK 2)

--Aidha, Dewe anapomsomea kwamba *'....Kamshina Henderson ametoa ahadi kwamba hatapumzika mpaka wauaji hawa, maharamia hawa....'*Musa anatema mate kwa hasira na kumtusu Kamishna akimwita mpumbavu! (UK 4)

--Bado kwa hasira, Katika mkutano wa wafanya-kazi tunamwona Musa anamrukia kwa ghafla MK na wanaanza kwa sababu MK amemtusu (UK 44)

--Bila shaka, Musa ni mvutaji sigara. Kwa mfano, wakati yeye na Dewe wanapokaa kuzumzia juu ya maisha ya wafanya-kazi, Musa anavuta sigara huku akitazama juu angani (UK1).

--Musa ni maskini na mwenye njaa. Kwa mfano, tunamwona akisema ati wanaishi kinyama Pia, anaendelea kusema ya kuwa wanashindana na mbwa na mapaka waking'ang'ania makombo yaliyotupwa mapipani na watu !(UK 1)

--Vile vile, Musa ni mchochezi wa mgomo, kwa mfano, tunamwona wakati anapoagana na Dewe baada ya mazungumzo yao, anasema, '*huu ndio mwanzo wa mwanzo. Huku ndiko kuzaliwa kupya. Twende ndugu! Twende...*' Anasema haya akiwa anakubaliana na ndugu yake Dewe kurudi nyumbani kuamsha wafanya- kazi kichinichini kuiendeza ka kazi ya Lanina (UK 6)

--Bila kudanganya, Musa ni shujaa, yaani; anatenda bila kuogopa, kwa mfano, tunamwona anaambia Delamon uso kwa uso kwamba hawataki tena hao wasaliti (*akintazama Tereki*) wawe wakuu wa chama chao (UK69). Anaendelea kumwambia kishujaa eti hawana haja ya huruma yake Delamon (UK 70)

--Isitoshe, Musa ni mzalendo yaani anaipenda nchi yake na yuko tayari kuigania uhuru na kuifia. Kwa mfano, tunamwona anaambia Delamon kuwa walinyosha mikono yao kijinga na kutiwa pingu lakini sasa wako tayari kuzitumia nguvu zao wenyewe kuzivunja..(UK 71)

--Musa lazima ni mfanya-kazi hodari yaani anafanya kazi katika shamba la Delamon (UK 43)

--Vile vile, Musa ni mwenye wasiwasi kwa mfano, tunamwona anasema, '*maisha yatakuwa taabu kupata kibarua*' (UK 1)

--Hatimaye Musa ni mpiganiaji haki ili aikomboe nchi yake dhidi ya udhalimu, ukandamizaji na unyanyasaji. Kwa mfano, tunamwona akiegemea swala / suala la kumtetea Lanina anapofungwa gerezani. Kwa mfano, tunamwona anajishikirisha katika mauaji ya Delamon, shindo na Tereki ili wakomboe nchi yao UK 72.

5. Tereki.

--Naye Tereki ni mfanya-kazi hodari. Kwa mfano, tunamwona anafanya kazi katika shamba la Delamon, mathalani, tunamwona amevalia nguo zake za kazi (UK 43)

--Ni mpigania haki. Kabla yake, Kula hongo, anaonekana na Lanina wakipigania haki zao kama vile kuandika malalamiko na kuyaleta kwa Delamon Pia, Tunamwona naye anashiriki katika kugoma (UK 12)

--Bila shaka Tereki ni msaliti kwa mfano anafungwa pamoja na Lanina jelani lakini anamsaliti na kula hongo. Kwa mfano, tunamwona anakubaliana na MK na wafanya-kazi wengine kuisaliti nchi yake kwa kumshabiki Delamon. Juu ya hayo, tunamwona baada ya kula hongo anamsihi Delamon kuwa ni kiongozi mzuri. Vile vile, yeye ni miongoni mwa wale wanaomshawishi Lanina kuacha migomo *UK (49-55)*

--Waidha, Tereki ni mvutaji sigara kwa mfano, tunamwona anawakaribisha wenzake kwa kuwapatia pakiti ya sigara (*UK 43*)

--Ni miognoni mwa viongozi wa chama cha wafanya- kazi shamba la Delamon (*UK 43*).

6. Mwengo.

Ni mumewe Lanina (*UK 29*) na babake Dida. Ana sifa zifuatazo;

--Kwanza, ni katili yaani anamtendea Lanina matendo bila huruma yoyote. Kwa mfano, tunamwona anaingia na bakora, anaanza kumpiga Lanina na kumwangusha chini huku watoto wakilia (*UK 55*).

--Vile vile, Mwengo ni mpenda utamaduni wake, kwa mfano tunamwona akisema kuwa Lanina ameacha utamaduni yaani kikwao, mke ndiye anayepaswa kumpikia mumewe (*UK 32*)

--Aidha, Mwengo ni mvutaji sigara, kwa mfano, tunamwona ndani ya chumba kidogo ameketi juu ya kochi anavuta sigara (*UK 29*)

--Fauka ya hayo, Mwengo ni mwenye ubabedume yaani haheshimu mke kwani tunamwona anaripoti Lanina kwa wazazi wake eti anatumia muda mrefu kwa wanaume na yeye hapewi muda (*UK 40*)

--Ghalibu, Mwengo ana wivi yaani anamwonea mkewe kijicho akimwona na wanaume wengine katika harakati za kupigania uhuru / haki. Kwa, mfano, tunamwona anampiga Lanina viboko kwa sababu amekuwa anazungumza na Pelekha, Matovu na Tereki (*UK 54*).

--Hali kadhalika, Mwengo ni mfanya-kazi kwa mfano, tunamwona Lanina akimwelezea eti ni mfanya- azi kama yeye na anazijua taabu na udhalimu na kuyakomesha hayo yote ni kupigania haki zao (*UK 31*).

--Vile vile, Mwengo ni mwepesi wa kukasirika yaani anapandwa na hasira ghafla anapokuta wanaume kwake na kushika bakora kuwafukuza (*UK 54*)

--Mwengo Lazima ni mwenye mapenzi kwa mfano, tunamwona anampapasa usoni mkewe Lanina anapokuta eti wamemteseka. Mathalani, tunamwona akimwomba msamaha kwa hamaki zake na mwishoni mwa onyesho wanashikana mikono na kuondoka (*UK 31-35*).

--Mwengo ni mvumilivu anayekosa mapenzi ya mke wake kwa muda mrefu lakini anavumilia. Na kwa hiyo, ni mvumilivu. Kwa mfano, tunamwona anabaki nyumbani na watoto akiwapikia chakula na kuwaosha. Kwa mfano, tunamwona akisema, 'mimi ndiye mpishi....' (UK 32)

7. Mama

Ni mamake Lanina

Ni Mkewe Baba. Ana sifa zifuatazo;

--Ni mwenye mapenzi yaani anamtetea mwanawe Lanina yaani tunamwona anamtetea dhidi ya matusi ya Baba, kwa mfano anamtetea akisema, '*Lanina sasa ana kazi mjini, watu lazima watamwonea kijicho...*' (UK 37)

--Vile vile, tunamwona anamkaribisha nyumbani akiangua kilio akimkimbilia mtotowe na kumkumbatia UK 37.

Juu ya mapenzi, tunamwona anamletea chakula na kumpa (UK 39).

--Mama kwa uhakika ni mtiifu kwa sababu anatii amri ya mumewe. Kwa mfano, anapoambiwa na mumewa Baba kumfunza mtotowe adadu anaitikia jambo hilo vema na kuanza kumfunza amri na adamu mtotowe (UK 39).

--Bila kudanganya, mama ni mpenda utamaduni kwa mfano, tunamwona anamfunza masuala ya utamaduni mtotowe kama vile ;anasema '*si umefunzwa kuwa mke daima awe chini ya mume? Lazima amtii na amhudumie mumewe!*'(UK 41).

8. Baba.

Ni babake Lanina na mumewe mama. Ana sifa zifuatazo;

--Ni mpenda utamaduni. kwa mfano, tunamwona akilalamikia Lanina eti amekuwa kijana wa kisasa anayejigeuza mzungu, pia anasema eti anataka kuwa mwanamume yaani amezitupilia mbali mila zao (UK 36)

--Pia, baba ni mvutaji sigara, yaani tunamwona anavuta tumbaku yake kidogo puani anachemua (UK 37)

--Aidha, ni mwenye ubabedume kwani tunamwona anataka mwanake Lanina aache mambo ya kujilinganisha na wanaume. Vile vile, tunamwona anamwambia Lanina ya kwamba ashike adhabu kwa sababu yeye ndiye simba wa nyumba yake na angurumapo hataki kusikia '*Lakini*' zake za kijinga .Anaendelea kumwambia eti asimwite wale wanaume wengine yaani yeye ni dume kweli kweli (UK 38)

--Bila shaka, Baba ni mkulima. Mathalani, tunaoma Lanina anatufafanulia eti babake ana kishamba chake, anapanda mahindi na mavuno yanamwendea vizuri ingawa wanamnunua kwa bei nafuu (UK 4)

--Aidha ni mkaidi. Kwa mfano tunamwona kimakusudi anamkataa mtoto wake. Mathalani, tunamwona anamwambia Lanina eti asimwite babake na ya kwamba yeye hawezi kuzaa shetani. Aidha, anaendelea kumwita Malaya(UK 37).

--Baba hali kadhalika ni mwenye wivu yaani hamtaki Lanina kujishughulisha na suala la kupigania haki za wafanya-kazi kwa sababu anadhani akienda pale anajishughulisha na wanaume wengine vivyo kuwa malaya.

--Hatimaye, Baba ni mwepesi wa kukasirika yaani tunamwona anapandwa na hasira ya karibu anawakabidhi na vipigo vikali Lanina na Mamake.

9. Zari

--Ni mfanyakazi hodari kwa mfano, tunaona anafanya-kazi katika shamba la Bw. Delamon (UK 7)

--Ni msaliti kwa sababu ni mwafrika angawa anajuunga na upande wa makaburu kuwanyanyasa waafrika wenzake (UK 8)

--Aidha, ni mwepesi wa kukasirika kwa mfano, tunamwona anapandwa na hasira ya karibu wakati wa kuwahoji Lanina na Tereki yaani tunamwona analaumu Lanina na Tereki kwa hasira kwa sababu wamechochea mgomo (UK 12)

--Bila shaka, Zari ni mwoga yaani tunamwona anatetema wakati Delamon anapomwambia kusikiliza sauti za wafanya-kazi wanaopiga kelele. Anaogopa na kushindwa kusema vizuri. Kwa mfano, anasema, 'Ni...ni...' (UK 8)

10. Shindo.

Ni mfanya-kazi anayefanya kazi katika shamba la Bwana Delamon (UK 7)

--Ni msaliti kwa sababu ni mwafrika lakini anajishughulisha na makaburu kuwadhalimu waafrika wenzake (UK 7)

--Ni mshwawishi kwa mfano, tunamwona anashawishi Lanina kuacha mgomo na kujiunga nao. Kwa mfano, tunamwona anashawishi Lanina kwamba Delamon ni mtu mwenye huruma na anamheshimu na anamtaka arudi kazini (UK 16)

--Vile vile, shindo ni mwenye kejeli yaani anatomia lugha ya kuwadharau waafrika, kwa mfano, baada ya Tereki kutoshawishika kwa kusema eti anataka muda wa kuyafiria mambo hayo, tunamwona anasema, *'waafrika wapumbavu sana. Mzungu huyu anajaribu kumsaidia na yeye ati anajidai anataka rufikiria kwanza . Kufikiria! Kufikiria! Ana akili gani za kufikiri, mshenzi yule!'*(UK 19).

11. Kachero wa 1 (Bwana Hatila)

--Ni mvutaji sigara, kwa mfano, tunamwona anapekuwa makaratasi anatoa paketi ya sigara mfukoni, anatoa sigara moja na kuishika baina ya vidole (UK 21)

--Pia, mhusika huyu ni mnyanyasaji kwa mfano, tunamwona anamnyanyasa Lanina kwa mfano, tunamwona Kachero wa 1 anavuta sigara na kuuzuia moshi ndani ya mapau kwa muda mfupi halafu kuuwachilia juu ya kichwa cha Lanina (UK 24)

--Juu ya unyanyasaji wake, tunamwona pia anampiga kofi Lanina ambalo linakingwa na Lanina lakini nguvu zake zinamwangusha chini anamwinamia na kujaribu kumpiga na kumshika koo (UK 25).

--Vivi hivi, ni Malaya kwa mfano anapeleka mikona yake juu ya mabega ya Lanina, na pole pole anaipoleka juu ya mashavu yake (UK 23)

12. Kachero wa 2

--Kwanza, huyu ni mpenda ubinafsi. Kwa mfano, anasema, 'hatuwezi *kumfanyia mpango kila kila mtu. Hii ni dunia ya ubinafsi*' (UK 26)

--Aidha, ni mshawishi, yaani tunamwona anamshawishi Lanina eti aerevuke kama Tereki ambaye amejiunga nao ingawa Lanina anakataa katakata (UK 27).

--Ni msaliti yaani ni mkazi wa nchi ya kifarika lakini anawasaliti wafanya -kazi wenzake kwa kushabiki Delamon (UK 23)

13. Henderson.

--Ni kamishna na mkuu wa polisi (UK 2)

--Ni mwepesi wa kukasirika yaani tunamwona anawaita maharamia wafanya -kazi wanaogoma (UK 4)

--Ni kiongozi yaani ni Kamshna mkuu (UK)

14. Mzee Mkongwe.

--Ni mwenye wasiwasi yaani tunamwona analamika juu ya njaa fisadi, laana ya miungu, uchungu wa dhiki(UK 5)

--Ni mzalendo mathalani, anaipenda nchi yake ndiyo sababu anailalamikia (UK 5)

15 .Kimbo

--Kwanza, ni mfanya- kazi wa Delamon (UK 9)

--Aidha, ni mwafrika msomi yaani ana uwezo wa kuzumgumza Kiigereza, baada ya kuitwa na Delamon yaani anasema, *'Yes-saa! Comin -saaa'* (U K9)

--Bila shaka, Kimbo ni maskini anayesumbuliwa vibaya na njaa. Kwa mifano, tunamwona anaonekana mnyonge.

16. Askari

--Bila kudanganya, huyu ni mkahaba. Mathalani tunamwona anamsongelea Lanina na kumrukia akijaribu kumbusu na kumpasulia nguo (UK 73)

17. Mzee Ingeli.

--Kwanza huyu ni mwenye huruma. Kwa mfano, tunamwona anamhurumia Lanina na kupa kazi baada ya kufukuzwa na Delamon (UK 56)

--Aidha, ni mfanya- biashara yaani ana biashara ya kioski ya kuuza uji na chai ambapo Lanina anapewa kazi (UK 56)

--Waidha, ni mwenye mapenzi. Kwa mfano, anampenda mjukuu wake Lanina. Mathalani tunamwona anampingia makofi akiwa anaimba wimbo wake wa kupigania haki za wafanya kazi (UK 56).

--Juu ya wanaume wanaoingia kupata uji anawaambia *'tena nisimwone mtu yeyote akimgusa mjukuu wangu au atakiona cha mtema kuni'* (UK 57)

--Naye Lazima ni Mzalendo yaani anaipenda nchi yake na kuwa tayari kupigania. Kwa mfano, tunamwona akimwuliza Lanina watakachofanya kuzuia unyanyasaji (UK 56)

18. Matovu

--Kwanza, ni mfanya- kazi katika shamba la Delamon yaani tunamwona na wafanya -kazi wenzake katika shamba la Delamon wakati wa mapumziko(UK 43).

--Aidha, ni mvutaji sigara yaani tunamwona anatoa au anachukua sigara anayopewe na Tereki (UK 43)

--Fauka, ni kiongozi yaani ni miongoni mwa viongozi wa wafanya- kazi wa chama chao cha kupigania haki zao (UK 43)

--Ghalibu, ni mpenda ubinafsi kwa mfano, tunamwona hapendi jambo la kumtetea mwenzake Lanina. Mathalani, anasema, *'hatuhwezi..... Hatuhwezi kujitia katika kila*

kitu sisi. Haki zetu za kikazi na siasa za Lanina ni....yaani..... si mambo yanayooana'(Uk 46)

--Bado juu ya ubinafsi, tunamwona anamwambia Lanina eti waanze wapigania nafsi zao kwanza, wajipatie vyeo, halafu wataweza kuwasaidia (UK 53)

--Hali kadhalika, ni msaliti yaani anawasaliti wafanya-kazi wenzake kwa kupigania nafsi zake mwenyewe (UK 50)

--Hatimaye, Matovu ni mwoga. Lanina anapowafukuza nyumbani mwake kwa ukali, tunamwona anajaribu kuribu nyuma anaanguka na kisimama haraka (Uk 52)

19. Pelekha

--Kwanza, Pelekha naye ni mfanya-kazi wa makaburu (UK 43)

--Juu ya hayo, ni kiongozi. Kwa mfano, tunamwona kama kiongozi majawapo wa viongozi wa chama cha wafanya- kazi (UK 43).

--Bila shaka, Pelekha ni msaliti yaani tunamwona anamshawishi Lanina eti waungane na wakasaliti wafanya-kazi wenzao kwa kumwambia Lanina suala ambalo limewaleta. MATHALANI, anasema'*Maadamu umeshaanza matovu, afadhali uendelee wewe! Endelea bwana! Endelea!*'(UK 50).

20. Mfanya- kazi (MK)

--Kwanza kabisa, ni mfanya-kazi katika shamba la Delamon (UK 43)

--Aidha, ni mvutaji sigara yaani tunamwona anachukua sigara zinazotolewa na Tereki (UK 43)

--Ghalibu ya hayo, ni mzazi. Kwa mfano, ana familia. Anatuonyesha kuwa hapendi migomo kwa sababu inaweza kuletea shida familia yake yaani mke na watoto wake (UK 46)

--Katika hali sambamba, MK ni msaliti yaani amekubuli nyongeza wanayopewa na Delamon ili waendelee kuwanyanyasa waafrika wenzake (UK 43)

--Bila kuenda mbali, MK ni mwenye kejeli yaani tunamwona katika mgogoro wake na Musa, anamtusu kwa kumwita kichaa (UK 44)

Maswali ya majaribio

1. *“Mada kilio cha haki inaoana na ujumbe uliomo katika tamthilia”*. Teta kauli hii ukitoa mifano kuntu kutoka tamthilia husika.
2. Linganisha na ulinganue maisha ya jamii yako na maisha ya *Kilio cha haki* ukitoa mifano maridhawa.
3. Elezea ploti ya tamthilia ya *kilio cha haki*
4. Kwa kutumia mifano dhahiri kutoka tamthilia *kilio cha haki* fafanua madhumuni / umuhimu wa wahusika wafuatao;(a)Lanina (b)Delamon(ch) Mama(d)Musa(e)Mwengo(f)Musa(g)Dewe. (h)Baba Fafanua mafunzo unayoyapata kutoka tamthilia *kilio cha haki*
5. Eleza jinsi mwanamke anavyosawiriwa katika tamthilia ya *kilio cha haki*. Toa hoja yenye mifano mwafaka.
6. Je, Lanina analinganishwa vipi na mwanamke wa jamii yako?
7. Fafanua jinsi wahusika wanavyopigania haki zao katika tamthilia ya *kilio cha haki* .Toa maelezo na mifano sahili.
8. *‘Wafanya-kazi wa kiafrika ndio wanaojiletea kunyanyaswa’*.Tetea kauli hii ukilinganisha mifano ya *kilio cha haki* na nchi yako.